# Kazi ya Sauli



Ellen White

# Kazi ya Sauli

Ellen White

Mfululizo wa Miswada kutoka kwa “Ishara za Nyakati”
Julai 13 – Sep 14 1882

Kwa maana kila kitu kilichoandikwa zamani, kiliandikwa kutufundisha, ili kwamba kwa saburi na faraja tunayopata katika Maandiko tuwe na tumainio. Warumi 15:4

Kimechapishwa na

MARANATHA MEDIA

maranathamedia.com

# Yaliyomo

1. Israeli Wanatamani Kuwa na Mfalme. ....................................................4

2. Mfalme Anateuliwa. ..........................................................................9

3. Uzinduzi katika Gilgali.....................................................................14

4. Dhabihu Iliyokataliwa. .....................................................................21

5. Ushindi wa Mikmashi .......................................................................24

6. Kiapo cha Haraka cha Mfalme Sauli. ................................................28

7. Watu waliopotoka. ............................................................................32

8. Jaribio la Mwisho. .............................................................................37

9. Kutii ni Bora Kuliko Dhabihu. ...........................................................43

# 1. Israeli Wanatamani kuwa na Mfalme.

**Mfumo wa kwanza wa serikali juu ya wanadamu ulianzishwa na Mungu mwenyewe, na ulimtambua yeye kama mfalme pekee**. Alifanya mapenzi yake yajulikane kwa amri zilizoandikwa na ufunuo, kwa ujumbe kwa watumishi wake wateule, kwa ndoto, kwa ishara, na miujiza. Angeendelea kuwa mfalme, kama wangeridhika na utunzaji wake wa kibaba.

**Hapo mwanzo, baba alikuwa kuhani na hakimu wa familia yake mwenyewe. Kisha kukaja utawala wa wazee, ambao ulikuwa kama huo wa familia, lakini ukapanuliwa kwa hesabu kubwa**. Waisraeli alipokuwa watu tofauti, kabila kumi na mbili, kutokea kwa wana kumi na wawili wa Yakobo, kila moja ilikuwa na kiongozi. Viongozi hawa, au wazee, walijumuika pamoja wakati suala lolote lenye kuhusiana na mambo ya jumla lilihitaji kushughulikiwa. Kuhani mkuu alikuwa mwakilishi anayeonekana wa Kristo, Mkombozi wa watu wake. Waebrania walipokaa Kanani, mahakimu waliteuliwa, ambao walifanana na magavana. Viongozi hawa walipewa uwezo wa kutangaza vita na kutangaza amani kwa taifa; lakini Mungu bado alitambuliwa kuwa Mfalme wa Israeli, na aliendelea kudhihirisha mapenzi yake kwa viongozi hawa teule, na kutangaza kupitia kwao uwezo wake.

**Lakini kuongezeka kwa watu, na kuingiliana na mataifa mengine, kulileta mabadiliko**. **Waisraeli waliridhi tamaduni nyingi za jirani zao wa mataifa, na kwa hivyo kwa kiwango kikubwa wakaacha, tabia yao ya kipekee takatifu. Ibada yao ikawa haina jitihada na ukweli. Hatua kwa hatua wakapoteza heshima yao kwa Mungu, na wakaacha kujivunia zawadi ya juu ya kuwa wateule wake**. **Wakilevyo na fahari na onyesho la wafalme wa mataifa, walichoshwa na unyenyekevu wao wenyewe, na wakatamani kuwekwa huru kutoka kwa uongozi wa Mfalme Mtakatifu**. **Walipojitenga kutoka kwa Bwana, makabila tofauti yakachukiana na kuwa na wivu kwa mengine**. **Ugomvi na mifarakano ikaongezeka, hadi ikafikiriwa kwamba kuwekwa kwa mfalme kulikuwa njia pekee ya kurejesha.**[1]

Serikali ya Israeli haikuwa imewahi endeshwa kwa hekima kuu na mafanikio kama wakati wa utawala wa Samweli pekee. Hakuna katika uongozi wa awali

[1] Hoja hii ni madhubuti sana kuishikilia. Uwepo wa mfalme ni tokeo la kujitenga na Bwana. Chuki na wivu ambazo zinazuka kutokana na kujitenga na Bwana zilimaanisha kwamba kama tu ufalme ungerejeshwa kwa uiano. Hili ndilo linalotendeka katika kanisa la Kiadventista. Limejitenga kutoka kwa Bwana na chuki na wivu zimekuwa zikichipuka na njia ya pekee ya kudumisha uiano ni kuwa na kamati ya kuweka amri na kuwaadhibu wale ambao hawatii.

watu walipumzika kwa imani thabiti. **Alikuwa ametenda kazi kwa bidii isiyokuwa na kikomo kwa uzuri wa taifa**. Katika kila shughuli alikuwa ameongozwa na haki na ukarimu. Na mwendo wake haukuwa tu wa kujikana nafsi, bali alikuwa mara kwa mara hakujali matakwa na haki yake mwenyewe. Kwa hivyo, ubinafsi uliodhihirishwa na wanawe ulionekana kugongana zaidi kwa upinzani na mwendo wa baba yao mwaminifu.

Kiburi na udhalimu wa mahakimu hawa ulisababisha kutoridhika kwingi miongoni mwa watu, ambao zaidi walisumbuliwa na hatari iliyokuwa ikitishia mahitaji yao ya muda kuliko walivyokuwa na uasherati na kufuru kwa Hophni na Phinehasi. Awali wengi ambao walijichukulia kukosea waliwasilisha malalamishi yao kwa wazee wa Isreali. Kisingizio basi kiliwekwa cha kusihi mabadiliko ambayo yalitamaniwa kitambo kwa siri.

**Kama Samweli angefahamishwa kuhusu udhalimu wa wanawe, mara moja angewaondoa, Wao, na kuwateua wengine, wema zaidi, mahali pao**. Wakati, hata hivyo, malalamishi dhidi ya wanawe yaliletwa mbele yake, yalifuatwa mara moja na ombi la mfalme, Samweli aliona kwamba nia ya kweli ilikuwa kutoridhika na kiburi. Alijua kwamba hamu haikutoka kwa msukumo wa ghafla, bali ilikuwa tokeo la maamuzi ya muda na kusudi lililoamuliwa.

Walalamishi walikuwa makini sana kusema kwamba hawakuona dosari katika utawala wa Samweli; lakini walisema kwamba hivi karibuni atakuwa mzee sana kuweza kuwahudumia, na wanawe walikuwa wamethibitisha kwamba hawawezi aminika. **Licha ya maelezo haya na fani ya kujali, Samweli aliumizwa sana. Aliona ombi hilo kama lawama juu yake, na jitihada za moja kwa moja za kumtenga**. Lakini hakuonyesha hisia zake. Hakutamka neno lolote la kukashifu kwa sababu ya kukosa shukrani kwa watu. Kama angefanya hili, neno moja chungu la dhambi lingeweza kufanya madhara makubwa.

Samweli alichukua suala hili jipya na nzito kwa Bwana katika maombi, na akatafuta ushauri kutoka kwake pekee. Maombi yake yalisikika; “Na Bwana akamwambia Samweli, **Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao.** Kwa kadiri ya matendo yote waliyonitenda tokea siku ile nilipowatoa katika Misri hata leo, kwa kuniacha mimi, na kwa kutumikia miungu mingine, ndivyo wanavyokutenda wewe.” **Nabii alikaripiwa kwa kuomboleza kwa matendo ya watu kwake yeye mwenyewe kama mtu binafsi**. Hawakuwa wameonyesha kukosa heshima kwake, bali kwa mamlaka ya Mungu, ambaye alikuwa ameteua viongozi wa watu wake.

Siku za mafanikio makubwa ya Israeli zilikuwa zile ambazo walimthamini Yehova kama mfalme wao,--wakati sheria na serikali ambayo alikuwa ameanzisha zilitambuliwa kuwa zenye nguvu kuliko zile za mataifa mengine yote. Musa mwenyewe kwa hotuba yake ya mwisho, alisihi wa Israeli, "Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama Bwana, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo?"

**Na ila, bila ya kujali Bwana mara nyingi alikuwa amefanya kwa nguvu kwa ukombozi wao, Waisraeli sasa walikuwa wamewekwa katika kuhusisha majanga yao yote na namna ya serikali yao**. Bwana aliruhusu watu wake wafuate mwenendo wao, kwa sababu walikataa kuongozwa na mashauri yake. **Hosea anatangaza kwamba Mungu aliwapa mfalme katika hasira yake**. Katika kiburi chao walitamani kuwa kama mataifa mengine, bila kuzingatia kwamba kwa fahari ya kifalme lazima pia wapitie dhuluma na malipo yake. **Hili litakuwa badilishano la uchungu na serikali ya upole na faida ya Mungu**.

Ni hatua hatari zaidi kuweka fimbo ya uongozi mkononi mwa mtu mwenye mwisho, na kumteua mfalme. Mungu huelewa moyo wa mwanadamu vyema zaidi kuliko jinsi wanadamu wenyewe huelewa. Kuondoka kutoka kwa mpangilio wa hekima wa Bwana kunaweza kugeuza utawala kuwa dhalimu, na kuwekwa katika utumwa. Hata kama watawala kiasilia walikuwa wenye huruma na wakarimu, nguvu nyingi juu ya wanadamu wenzake zinaweza mfanya dhalimu. Nguvu kama hizo ni Mungu tu anaweza zitumia kwa haki na hekima.

**Bwana alikuwa, kupitia kwa manabii wake, ametabiri kwamba Israeli watatawaliwa na mfalme. Lakini hakuna kwa vyovyote vile inafuata kwamba aina hii ya serikali ilikuwa kulingana na mapenzi yake. Ingawa huwa anaona mambo yote awali, mara nyingi huruhusu wanadamu kufuata mwenendo wao wenyewe, wanapokataa kuongozwa na mashauri ya hekima isiyo na mwisho**. Katika hatua hii, alimwagiza Samweli kuwatimizia ombi lao. Lakini kwa uaminifu awaonye kuhusu kutoidhinishwa na Bwana, na pia kuwajuza kile ambacho kitakuwa tokea la mwenendo wao: "Basi sasa, isikilize sauti yao; walakini, uwaonye sana, na kuwaonyesha desturi ya mfalme atakayewamiliki."

Samweli ipasavyo aliwakusanya watu, na kwa imani akawasilisha kwao mizigo ambayo watabeba chini ya mfalme, na tofauti kati ya hali kama hiyo ya ukandamizwaji na hali yao ya sasa huru na ya mafanikio. Aliwakumbusha kwamba mfalme wao ataiga fahari na anasa ya wafalme wengine, kuunga kile ambacho, ni madai mabaya kwa watu wao na mali kutahitajika. Atawachukua vijana wadogo kuwa wapanda farasi, na hata ataajiri baadhi kuendesha magari

yake ya farasi. Jeshi imara litahitaji huduma zao; na pia watahitajika kulima shamba lake, kuvuna mazao yake, na kutengeneza kwa huduma yake zana za vita.

Binti za Israeli, ambao wangekuwa msingi wa boma zenye furaha, watachukuliwa kuwa wapishi na waokaji, kuhudumu kwa anasa za nyumba ya mfalme. Kuunga mkono hali yake ya kifalme atatafuta kisingizio cha kuchukua mashamba yao mazuri, yaliyopeanwa kwa watu na Yehova. Watumishi wao wazuri pia, na ng'ombe wao, atawachukua na "atawatia katika kazi zake mwenyewe."

Kando na haya yote, ushuru wa kukandamiza utawekwa. Watu tayari walimpa Bwana fungu la kumi la kipato chao, faida ya kazi yao, au mazao ya ardhi. Mfalme atahitaji fungu zaidi kwa vyote. "Nanyi mtakuwa watumwa wake," akahitimisha nabii. "Nanyi mtalia siku ile kwa sababu ya mfalme wenu mliyejichagulia; Bwana asiwajibu siku ile."

Lakini watu walikuwa wameegemea katika kufuata mwenendo wao wenyewe. Maonyo wazi kutoka kwa Mungu, kupitia kwa nabii wake mkongwe, hayakuwa na athari ya kuwageuza kutoka kwa kusudi lao. Walirejesha jibu, "Sivyo hivyo; lakini tunataka kuwa na mfalme juu yetu; ili sisi nasi tufanane na mataifa yote; tena ili mfalme wetu atuamue, tena atoke mbele yetu na kutupigia vita vyetu."

"Tufanane na mataifa yote"—Waisraeli hawakutambua kwamba kuwa katika heshima hii tofauti na mataifa mengine ilikuwa fadhila ya kipekee na baraka. Mungu alikuwa ametenga Israeli kutoka kwa mataifa mengine yote, kuwafanya hazina teule yake mwenyewe. Lakini wao, wakipuuza heshima hii kuu, kwa hamu walitamani kuiga mfano wa mataifa. Ni upofu wa namna gani! Ni ukosefu wa shukurani namna gani!

Kwa huzuni nyingi, Samweli alisikiliza maneno ya watu, na kisha tena akatafuta mwelekezo wa uungu. Na Bwana akamwambia Samweli, "Isikilize sauti yao, ukawafanyie mfalme."

Nabii alikuwa ametekeleza wajibu wake. Alikuwa amewasilisha maonyo kwa imani, na yalikuwa yamekataliwa. Hangesema zaidi. Kwa moyo mzito aliwatawanya watu, naye mwenyewe akaondoka kuandaa mabadiliko makubwa katika utawala.

**Inawezekana kifungu hiki katika historia ya Israeli hakikuwa na mwenzake katika uzoefu wa sasa wa watu wa Mungu! Hamu ya badiliko isiyokubalika,**

**matamanio ya kuendana na mipango ya ulimwengu na tamaduni za ulimwengu, mara nyingi hudhibiti wanaodai kuwa Wakristo**. Wanapoondoka kutoka kwa Mungu, wanakuwa na tama ya faida na heshima ya ulimwengu. Wale ambao husimama dhabiti dhidi ya kufanana na ulimwengu, kiburi cha kufisha moyo, ziada ya mali, na ubadhirifu, na kuangazia unyenyekevu na kujikana nafsi, huonekana kuwa muhimu, wateule, na sahihi. Baadhi hudai kwamba kwa kuunganika na ulimwengu na kufanana na tamaduni zao, Wakristo wanaweza leta athari kubwa ulimwenguni. Lakini wale wote ambao hufuata mkondo huu hujitenga kutoka kwa chemchemi ya uwezo wao. Kuwa rafiki wa dunia, wanakuwa adui wa Mungu.

Matamanio yasiyoridhishwa ya nguvu za kidunia na maonyesho, ni ngumu kuyatibu sasa kama ilivyokuwa katika siku za Samweli. Wakristo hutafuta kujenga kama walimwengu wajengavyo, kuvalia kama walimwengu wanavyovalia,--kuiga tamaduni na matendo ya wale wanaomwabudu mungu wa ulimwengu huu. Maagizo ya neno la Mungu, mashauri na makaripio ya watumishi wake, na hata maonyo yanayotumwa moja kwa moja kutoka kwa Enzi yake, yanaonekana kutokuwa na nguvu za kutiisha matarajio haya yasiyofaa kitu. Wakati moyo umefungwa kutoka kwa Mungu, karibu kisingizio chochote kinatosha kuhalalisha kupuuza mamlaka yake. Hamasisho la kiburi na kujipenda kunafurahiwa kwa gharama yoyote kwa sababu ya Mungu.

Kutotakasika na kupenda ulimwengu daima ziko tayari kukosoa na kulaumu wale ambao wamesimama bila hofu kwa Mungu na haki. Kasoro ikionekana kwa yule ambaye Mungu amemutwika jukumu kubwa, basi ibada yake yote ya awali inasahaulika, na juhudi ya kunyamazisha sauti yake inafanywa na kuharibu athari yake. Lakini mahakimu hawa wa kujiweka na wakumbuke kwamba Bwana huisoma mioyo. Hawawezi ficha siri yake isionekane na mtazamo wake wa utafiti. Mungu anatangaza kwamba ataleta kila tendo katika hukumu, na hata kila tendo la siri.

Watu muhimu sana wanathaminiwa kwa nadra. Wale ambao wamefanya kazi kwa bidii zaidi na kwa kujikana nafsi kwa wenzao, na wale ambao wamekuwa muhimu katika kuafikia makuu, mara nyingi wanalipwa kwa ukosefu wa shukrani na kupuuzwa. Watu kama hao wanapojipata wametengwa, mashauri yao kudunishwa na kudharauliwa, wanaweza hisi kuwa wanapitia dhuluma kuu. Lakini na wajifunze kutoka kwa mfano wa Samweli sio kujihalalisha au kujithibitisha, isipokuwa Roho wa Bwana bila hatia hupendekeza mkondo kama huo. Wale ambao hudharau na kukataa watumishi waaminifu wa Mungu, hawaonyeshi dharau kwa mtu huyo tu, bali

kwa Bwana aliyemtuma. Ni maneno ya Mungu, maonyo na ushauri, ambayo yanafanywa bure; mamlaka yake yanayokataliwa.

**Watu wanapozidi katika kufuata mienendo yao wenyewe, bila kutafuta mashauri kutoka kwa Bwana, mara nyingi huwapa matakwa yao, ili kuonyesha upumbavu au adhabu ya uovu wao**.[2] Wanapochukulia kwa mzaha maneno ya watumishi wake, anaweza ruhusu sauti ya ushauri na maonyo inyamazishwe. Lakini kiburi na hekima ya wanadamu itapatikana kuwa mwongozo hatari. Kile ambacho hutamaniwa zaidi na moyo ambao haujatakasika kitathibitisha kuwa chungu mno na cha kuhuzunisha hatimaye.

Wacha watumishi wa Mungu wabebe mizigo yao hadi kwa mkombozi wao mwenye huruma. Sikio lake li wazi daima kwa maombi yao. Jicho lake hutambua kila dhabihu na kila huzuni. Kukataliwa na dhuluma ambazo huwa wanapitia hapa zitafanya zawadi yao kuwa kuu katika siku ijayo.

## 2. Mfalme Anateuliwa.

Ingawa mfumo wa utawala wa kifalme kwa Israeli ulikuwa umetabiriwa katika unabii, sheria zilikuwa zimewekwa kwamba wale tu ambao watakwezwa kwenye enzi ni wale ambao wamechaguliwa na Yehova mwenyewe. **Waebrania bado waliheshimu mamlaka ya Mungu kiasi cha kuacha uteuzi mikononi mwake kabisa**. Uteuzi ulimwangukia Sauli, Mwana wa Kish, wa kabila la Benyamini.

**Sifa za kibinafsi za mfalme wa baadaye zilikuwa kama kufurahia kiburi hicho cha moyo ambacho kilisababisha tama ya mfalme**.[3] Hakukuwa na mtu mzuri zaidi kumliko miongoni mwa watu wote wa vilima. Mwenye heshima na cheo, katika ukuu wote wa maisha, mtulivu na mrefu, alionekana kama aliyezaliwa kuamrisha. Ingawa hata akiwa na vivutio hivi vya nje, **Sauli alikuwa fukara wa sifa za juu ambazo hujenga hekima ya kweli. Hakuwa amejifunza**

[2] Na itambulike kwamba Mungu alikuwa akiwaadhibu Waisraeli kwa kuwapa Mfalme Sauli. Huu ni mfano wazi wa tukio la kuadhibu dhambi kwa dhambi.

[3] Waisraeli wanaacha uteuzi wa mfalme kwa Mungu na Mungu anawapa mfalme ambaye wanatamani. Hii kanuni ya kioo ikitenda kazi. Yakobo 1:23. Tazama pia Agape sura ya 9. Sheria kama Kioo. Mungu anadhihirisha kwao kilicho mioyoni mwao kwa kuwapa kile ambacho wanatamani. Hili ni thibitisho zaidi kuwa hawapo katika agano la milele. Hawako katika Kristo bali katika Agano la Kale la tamaa zao wenyewe.

**katika ujana wake kudhibiti tama ya hasira yake ya haraka; kamwe hakuwa amehisi nguvu za neema takatifu**.[4]

Sauli alikuwa mwana wa kiongozi mwenye nguvu na tajiri, ila kulingana na unyenyekevu wa enzi hizo, alishirikiana na baba yake katika majukumu ya chini ya ukulima. Kundi la ng'ombe wa baba likiwalimepotea kwenye mlima, Sauli alitumwa pamoja na mtumishi wakalitafute. Kwa siku tatu kazi hiyo haikuzaa matunda, na kisha, wakajipata karibu na Rama, nyumbani mwa Samweli, mtumishi alipendekeza waulize kutoka kwa nabii kuhusiana na mali iliyopotea: "mkononi mwangu nina robo ya shekeli ya fedha; nitampa huyo mtu wa Mungu fedha hiyo, atuambie njia yetu." Hii haikuwa kama hongo; ilikuwa desturi kwa mtu akimwendea mwenye cheo au ofisi ampe zawadi ndogo, kama njia ya kuonyesha adabu na heshima.

Wakikaribia mji, waliulizia mwonaji, kwa wasichana wachanga waliokuwa wamekuja kuteka maji. Katika jibu walifahamishwa kwamba huduma ya kidini ilikuwa karibu kutendeka, na kwamba hakimu tayari alikuwa amewasili, kungekuwa na kafara "mahali pa juu," na baada ya hilo sherehe ya mteule.

Badiliko kubwa lilikuwa limetendeka chini ya uongozi wa Samweli. Ibada ya Mungu ilikuwa imedumishwa katika nchi yote, na watu walidhihirisha hamu katika huduma ya kidini. Sanduku likiwa bado linasalia Kirjath-jearim, na kukiwa hakuna huduma katika hema, kafara kwa wakati huo zilitolewa mahali pengine; na miji ya makuhani na walawi, mahali ambapo watu walirejeshwa kwa maagizo, kuliteuliwa kwa kazi hii. Mahali pa ju katika miji hii kwa kawaida kuliteuliwa kuwa mahali pa kafara, na kwa hivyo kulitawala "mahali pa juu."

Kwa tukio la sasa kafara ya amani ingewasilishwa mbele za Bwana, kwa ombi la bidii ili ikubalike, na kwa mibaraka yake kwa ibada kama njia ya uzuri wa kiroho kwa waabuduo. Kisha, Baraka imetenguliwa juu ya sehemu hiyo ya kafara ambayo ilikuwa imewekwa kwa ajili ya watu, wote wangeunganika kwa sherehe takatifu. Alipokuwa akianzisha mfumo wa dini za nje, Saweli alijaribu kuhimiza roho ya ibada ya kweli. Huduma hizi hazikuwa zinaruhusiwa kushusha tu kwa sherehe, au kuwa fursa ya kujiinua nafsi. Zikifanywa kwa urahisi, zilikuza ucha Mungu na pia roho ya ukarimu na huruma miongoni mwa watu.

Kwenye lango la mji, Sauli alikaribishwa na nabii mwenyewe. Mungu alikuwa amemfunulia Samweli kwamba siku hiyo na saa hiyo mfalme teule wa

[4] Sauli hakuwa mtu mwongofu. Kamwe hakuwa amehisi uwezo wa kufanywa upya wa neema takatifu. Alikuwa onyesho la viongozi wa taifa.

Israeli atajiwasilisha mbele zake. Sasa waliposimama ana kwa ana, Bwana alimwambia Samweli, “Huyu ndiye niliyekuambia habari zake; huyu ndiye atakayewamiliki watu wangu.”

Ombi la Sauli, “Tafadhali, uniambie, nyumba ya mwonaji iko wapi,” Samweli akajibu, “Mimi ndimi mwonaji,” akimhakikishia kwamba baba yake pia alikuwa amepata ng’omba aliyepotea, na sasa alikuwa ameanza kuwa na wasiwasi na mwanawe. Hata hivyo, alimsihi akae naye na ahudhurie sherehe, wakati huo huo akimpa baadhi ya vidokezo vya hatima kuu mbele yake.

Sauli akajibu, kwa kujishusha kwa kawaida. “Je! Mimi si Mbenyamini, mtu wa kabila iliyo ndogo kuliko kabila zote za Israeli? Na jamaa yangu nayo si ndogo kuliko jamaa zote za kabila ya Benyamini? Kwa nini basi, kuniambia hivyo?

Karibu watu thelathini wenye msimamo wa mji walikuwa wamealikwa kuhudhuria sherehe, na Samweli alimwongoza mgeni kwa chumba ambacho wageni hawa walikuwa wamekusanyika, akampa kiti cha heshima, na chakula kilipopakuliwa aliagiza kuwa kiungo cha kuheshimiwa, bega, kiwekwe mbele yake.

Aliporudi nyumbani kwake mjini, Samweli alijumuika na wageni wake darini, kama pahali patulivu na pweke, na hapo akanena nao, akiweka mbele yao kanuni kuu ambazo Serikali ya Israeli ilikuwa imejengwa juu yake, na kwa hivyo akitafuta kumuandaa kwa kiasi fulani kwa cheo chake kikuu.

Sauli alipoondoka, mapema asubuhi iliyofuatia, nabii alitembea pamoja naye. Baada ya muda, Samweli alimwagiza mtumishi kuendelea mbele, na kisha akamwagiza **Sauli asimame wima ili aweze kumuonyesha kusudi la Mungu**,[5] alimteua nahodha wa urithi wa Bwana. Kisha akambusu, na kufanya imani yake iwe dhabiti, alimwambia kwa usahihi wa hali ya juu matukio kadhaa ambayo yatatendeka katika safari ya kuelekea nyumbani, na kumhakikishia kwamba atahitimishwa na roho wa Mungu kwa vituo muhimu ambavyo vinamsubiri.

[5] Kwa kuzingatia kanuni ya kusudi la Mungu tunasoma kwa hamu tukio lingine. “Unabii wa Nuhu haukuwa tu hukumu ya kiholela ya ghadhabu ya Mungu au tangazo la mapendeleo. Haukurekebisha tabia na hatima ya wanawe. Bali ulionyesha kile ambacho kitakuwa tokea la mwenendo wa maisha ambayo walikuwa wamechukua mara kadhaa na tabia walizokuwa wamekuza. **Lilikuwa onyesho la kusudi la Mungu kwao na vizazi vyao kwa mtazamo wa tabia na mienendo yao**.” PP 118.2

Sauli alipoenda zake, alishuhudia utimizwaji wa maneno ya nabii, karibu na kaburi la Raheli, katika mpaka wa Benyamini, alifahamishwa kuwa wanyama waliopotea wameonekana. Katika mwaloni wa Tabori alikutana na watu watatu waliokuwa wakisafiri kwa mlima mtakatifu huko Betheli, kumwabudu Mungu. Mmoja alikuwa akibeba wana-mbuzi watatu wa sadaka, mwingine mikate mitatu, na wa tatu kiriba cha divai. Walimpa Sauli salamu za kawaida, na wakampa mikate miwili.

Sauli alipofika Gibea katika Benyamini, alisikia kundi la manabii likirejea kutoka mahali pa juu ambapo walikuwa kuabudu; na walipokuwa wakitembea, waliimba utukufu wa Mungu kwa kinanda na tari, kinubi na firimbi. Kisha Roho wa Mungu akamjilia Sauli, na pamoja nao akaimba nyimbo za utukufu na akatangaza maajabu ya ukweli mtakatifu. Alizungumza kwa ufasaha na hekima kubwa, na akaunganika kwa bidii  katika huduma ya maombi na kusifu, kiasi kwamba wale ambao walimjua tu kama mkulima walishangaa kwa ajabu, "ndipo watu wakasemezana, Ni nini hilo lililompata mwana wa Kishi? Je! Sauli pia yumo miongoni mwa manabii?" hawakuweza kuelewa jinsi badiliko hili kubwa lilikuwa limetekelezwa.

Samweli alikuwa ameanzisha ukuzwaji wa kawaida wa kwanza kwa maelekezo ya kidini na kufunuliwa kwa vipawa vya unabii. Miongoni mwa masomo ya msingi, kulikuwa na sheria ya Mungu na maagizo yaliyotolewa kwa Musa, history takatifu, nyimbo takatifu, na mashairi. Katika hizi "shule za manabii" vijana walifundishwa na wale walifahamiana tu na ukweli takatifu, bali ambao wenyewe walidumisha ushirika wa karibu na Mungu na walikuwa wamepokea urithi wa kipekee kutoka kwa Roho. Waelimishaji hawa walifurahia heshima na imani ya watu ya kujifunza na ucha Mungu. Nguvu za Roho Mtakatifu mara kwa mara zilikuwa zikijidhihirisha katika mikutano yao, na kazi ya vipawa vya unabii haikuwa nadra. Shule hizi, au vyuo, zilikuwa na thamani isiyoelezeka kwa Israeli, sio kwa usambazaji wa ukweli wa kidini, bali kwa kuhifadhi roho muhimu ya uungu.

Sauli alipojumuika na manabii katika ibada yao, badiliko kuu lilifanywa ndani yake na nguvu za kuhuisha za Roho Mtakatifu. **Nuru ya utukufu na utakatifu iliangaza katika giza la uharibifu wa maadilia. Alijiona jinsi alivyokuwa mbele za Mungu. Aliona na akahisi uzuri wa utakatifu. Sasa alikuwa aanze kwa bidii vita dhidi ya dhambi na Shetani, na alikuwa amefanywa kuhisi kwamba katika mgogoro huu nguvu zake lazima zije kutoka kwa Mungu kikamilifu. Mpango wa ukombozi, ambao awali ulikuwa umeonekana kufifia na kukosa uhakika, ulifunuliwa kwa ufahamu wake kwa uwazi mkubwa na nguvu**.

Uzoefu ambao baadhi ya Wakristo wamekuwa wakipata kwa miaka Sauli aliupata kwa muda mfupi. Bwana alimjalia ujasiri na hekima kwa cheo chake cha juu. **Alimdhihirishia chemchemi ya nguvu na neema, na kisha, akiwa ameangaza ufahamu wake kwa madai takatifu, na wajibu wake mwenyewe, alimwacha huru kutii nuru ambayo alikuwa amepokea**.

Ukweli kwamba Sauli alikuwa ameteuliwa kuwa mfalme juu ya Israeli haukufanywa kujilikana kwa taifa. Uteuzi wa Mungu ungedhihirishwa kwa umma kupitia kwa kura. Kwa sababu ya kusudi hili Samweli aliwakusanya watu Mizpeh. Ombi la bidii lilitolewa kwa uongozi mtakatifu; kisha ikafuata sherehe ya kupiga kura. Kwa kimya cha kutwetatweta umati uliokusanyika ulisubiri suala hili. Kabila, familia, na boma ziliteuliwa kwa mfululizo, na kisha sauli, mwana wa Kishi, alichaguliwa kama aliyeteuliwa. Lakini Sauli hakupatikana. Akihakikishiwa matokeo, na akitwishwa mzigo wa hisia za majukumu mazito ambayo karibu yanamwangukia, alikuwa amejitenga kutoka kwa umati.

Wakati kurejea nyuma kwake kuligunduliwa, aliletwa mbele ya umati, na walitazama kwa kiburi na kuridhika kwamba alikuwa na umbo la kifalme na cheo, kwa vile “alikuwa mrefu kuliko watu wote, tangu mabega yake kwenda juu.” Na kisha samweli akamtangaza kwa umati kwa maneno, “Mnamwona mtu huyu aliyechaguliwa na Bwana, ya kuwa hakuna mtu mfano wake katika watu wote!” katika kuitikia maneno yake, kelele kubwa ya furaha ilizuka kutoka kwa kundi hilo kubwa, “Mfalme na aishi!”

Samweli kisha akaweka mbele ya watu “jinsi ya ufalme,” akisema kanuni ambazo serikali ya kifalme ilikuwa imewekwa kwa misingi yao, na ambazo itadhibitiwa nazo. Mfalme hakupaswa kuwa mwenye nguvu zaidi, bali awe na nguvu zake kwa unyenyekevu kwa mapenzi ya Aliye Juu. Hotuba hii ilirekodiwa katika kitabu, ambapo kuliwekwa majukumu ya mfalme na upendeleo utakao pewa watu. Samweli alijua kwamba mfalme angeegemea kuchukua mamlaka yasiyofaa, na akalinda kadri iwezekanavyo uhuru wa taifa.

Watu kwa jumla walikuwa wamemtambua Sauli kama mfalme wao, na wakamletea zawadi kama vile wafalme wa Mashariki hupokea kwa kawaida. Lakini bado kulikuwa na wale ambao hawakufurahia na kuridhika. **Kwamba mfalme anaweza teuliwa kutoka Benyamini, kabila ndogo kabisa katika Israeli, na kupuuza Yuda na Ephraimu, makabila yenye watu wengi na nguvu zaidi, lilikuwa kosa ambalo hawawezi zuia. Walikataa kutangaza heshima kwa Sauli au kumletea zawadi za kitamaduni**. Hata hivyo aligundua dharau zao, lakini kwa hekima “akadumisha amani yake.” Katika hali iliyokuwepo ya mambo hakuona vyema kuchukua heshima na nguvu za kifalme. Akimuacha

Samweli akiongoza kama awali; alirejea nyumbani mwake Gibea. Alisindikizwa huko kwa heshima na kundi, ambalo, liliona uteuzi mtakatifu katika uamuzi wake, walikuwa wameamua kumhifadhi.

**Wale ambao walikuwa wakwanza kabisa katika kuitisha mfalme, ndio wale waliokataa kukubali kwa shukrani mtu aliyeteuliwa na Mungu. Matarajio yao hayakutambuliwa**. Walitazamia mfalme aapishwe kwa fahari na onyesho kubwa; kwa kukosa hili, walihisi kwamba machache yamepatikana. **Chuki na wivu zilichoma katika mioyo ya wengi. Kila mmoja alikuwa na aliyependa ambaye alitamani kuona katika kiti, na wengine miongoni mwa viongozi walikuwa wametamani kuchukua nafasi katika cheo cha juu**. Jitihada zote za kiburi na tamaa zilikuwa zimepelekea kwa masikitiko na kutoridhika. Ndivyo ilivyo daima. Moyo lazima ujifunze kunyenyekea kwa Mungu, ili kuwa na amani.

## 3. Uzinduzi Katika Gilgali

Sauli alikuwa ameteuliwa na Mungu na kuthaminiwa na taifa kama mfalme wa Israeli; ila hakufanya jaribio lolote la kuhifadhi haki yake kwenye enzi. Nyumbani mwao miongoni mwa milima ya Benyamini kimyakimya alijihusisha na kazi ya ukulima, na akaacha kuanzishwa kwa utawala wake mikononi mwa Mungu kabisa. Haikuhairishwa kwa muda mrefu. Pindi tu baada ya kuchaguliwa kwake, Waammoni, chini ya mfalme wao, Nahashi, walivamia himaya iliyozozaniwa mashariki mwa Yordani, na wakatishia mji mkubwa na wenye nguvu wa Jabesh-gileadi. Wakaazi walijaribu kupata mazungumzo ya amani kwa kujitoa kuwa tawi la Waammoni. Lakini mfalme mshenzi na katili alikataa kuwahifadhi, ila kwa masharti kuwa lazima aondoe jicho la kulia la kila mmoja wao, ili yasalie kama minara mingi hai ya utawala wake.

Watu wa mji uliohasiriwa waliomba kipindi cha siku saba za mashauriano, wakitarajia kwamba katika kipindi hiki makabila ya magharibi ya mto yanaweza itwa kwa ukombozi wao. Waammoni walikubali, wakiamini kwamba kama suala hilo litafanywa kuwa la umma litaongeza heshima yao sana kwa ushindi waliokuwa wanatarajia.

Wajumbe wepesi walieneza mawimbi kote Israeli, yakizua hofu na bumbuazi kila mahali. Sauli, akirejesha mifugo wake kutoka malishoni, alisikia kilio kikubwa kilichoashiria janga kubwa. Alisema, “Watu hawa wana nini, hata wakalia?” kisa cha aibu kiliporudiwa, nguvu zake zote zilizokuwa zimetulia

ziliamshwa, akasimama kama shujaa na mfalme. **"Na roho ya Mungu ikamjilia," kama vile kwa Samsoni, "Naye akatwaa jozi ya ng'ombe, <u>akawakata-kata vipande</u>, kisha akavipeleka vile vipande mipakani mwote mwa Israeli kwa mikono ya wajumbe, kusema, Ye yote asiyetoka nyuma ya Sauli na Samweli, ng'ombe zake watatendwa vivi hivi."**

Waisraeli wote walitii. Watu elfu mia tatu na thelathini walikusanyika katika bonde la Bezeki, chini ya amri ya Sauli. Kisha wajumbe wakatumwa mara moja wakawafahamishe watu wa Yabeshi-gileadi kwamba wanaweza hitaji msaada kesho, siku hasa ambayo wangewatazama Waammoni.

Kwa kuandamana usiku kucha, mfalme pamoja na jeshi lake alifika mbele ya Yabeshi-gileadi asubuhi. Kisha akagawa jeshi lake katika makundi matatu, ambayo yalisongelea kambi la waammoni kutoka pande tofauti, na kufanya mashambulizi ya ghafla na makubwa, wakawaondoa kabisa, kwa mauaji makubwa. Wale ambao waliponea walitawanyika kiasi kwamba wawili hawangeonekana pamoja.

Kwa haraka na nguvu ya mfalme juu ya tukio hili, na vile vile ujasiri na ujuzi wa kijeshi, watu walikuwa wameathiriwa zaidi kwa upendeleo wake kuliko walivyokuwa kwa uteuzi wa Bwana, upako wa Samweli, au kuonekana kwake kwa kupendeza. **Sasa, kwa sauti moja, walimsalimia kama mfalme wao, wakihusisha heshima yote ya ushindi kwa ujuzi wa mwanadamu, na kusahau kwamba bila mibaraka ya Pekee ya Mungu juhudi zao zote zingekuwa bure.**

Katika shauku yao, baadhi yao walipendekeza kuwaua wale ambao mwanzo walikuwa wamekataa kunyenyekea kwa utawala mpya. Lakini mfalme akaingilia, akisema, "Hakuna mtu atakayeuawa leo, maana leo Bwana amefanya wokovu katika Israeli." **Hapa Sauli alitoa ushahidi wa badiliko kuu ambalo lilikuwa limetendeka katika tabia yake. Badala ya kujichukulia heshima, alimpa Mungu utukufu, ambao kwa haki ulikuwa wake**. Badala ya kuonyesha hamu ya kulipiza kisasi, kwa kawaida, alidhihirisha roho ya huruma na kusamehe. **Huu ni ushahidi dhabiti kwamba neema ya Mungu inakaa moyoni.**

Samweli sasa alipendekeza kwamba watu waende Gilgali, na kwa heshima wathibitishe ufalme kwa Sauli, **upinzani wote kwa utawala ukionekana sasa umekoma**.[6] Hili lilifanywa, kwa furaha kuu, na sadaka nyingi za shukurani.

Gilgali palikumbukwa kama mahali pa kwanza pa kupiga kambi pa Israeli katika nchi ya ahadi. Hapa Yoshua aliweka nguzo ya mawe kumi na mawili kukumbuka kuvuka Yordani kwa muujiza; hapa manna ilikoma; hapa kutahiriwa kulirejeshwa; hapa watu walitunza pasaka ya kwanza baada ya kutangatanga kwao; hapa Nahodha wa Jeshi la Bwana alijitokeza. Tokea mahali hapa walikwenda kupindua Yericho na kuwashinda Ai. Hapa Akani alikutana na ghadhabu kali ya dhambi yake, na hapa mkataba usiokuwa wa busara ulifanywa na Wagibioni ambao uliadhibu mapuuza ya Israeli ya kuagiza ushauri wa Mungu. Juu ya tambarare hii, yenye utajiri katika muungano wa kusisimua, walisimama Samweli na Sauli; na wakati kelele za makaribisho kwa mfalme zilikuwa zimefifia, nabii mkongwe alinena kwa watu maneno yake ya kuwaaga kama mtawala wa taifa.

Mibaraka iliyopeanwa kwa Israeli isije ikawaongoza katika kuhalalisha uendeleo wao wote, Samweli alichukua fursa hii kuwashauri kwamba mwendo wao haukuwa unampendeza Mungu zaidi. Pia alithibitisha tabia yake mwenyewe na usafi wa utawala wake. Alifanya wito kwa watu kuonyesha hata tukio moja la udanganyifu, ukandamizaji, au ufisadi, wakati yeye pekee alikuwa hakimu wao:--

"Kisha Samweli akawaambia Israeli wote, Angalieni, nimeisikiliza sauti yenu katika hayo yote mliyoniambia, nami nimemtawaza mfalme juu yenu. Basi sasa, angalieni, mfalme anakwenda mbele yenu; na mimi ni mzee, mwenye mvi; tena, tazameni, wana wangu wapo pamoja nanyi; nami nimekwenda mbele yenu toka ujana wangu hata leo. Nami nipo hapa; basi, mnishuhudie mbele za Bwana, na mbele ya masihi wake, nalitwaa ng`ombe wa nani? au nalitwaa punda wa nani? au ni nani niliye mdhulumu? Ni nani niliyemwonea? Au kwa mkono wa nani nimepokea rushwa inipofushe macho? Nami nitawarudishia ninyi."

---

[6] Watu wa Israeli sasa wanamkubali Sauli kwa sababu ya kazi yake na sio kwa sababu Samweli alikuwa ameashiria awali kuwa alikuwa ameteuliwa. Hili ni thibitisho zaidi la uasi wao dhidi ya kumwamini tu Mungu.

Bila hata sauti moja pinzani, watu wakajibu, "Nao wakasema, hukutudhulumu, wala hukutuonea, wala hukupokea kitu kwa mkono wa mtu awaye yote."

Samweli alikuwa na kitu cha cheo zaidi kuliko tu kuhalalisha mwendo wake mwenyewe. Awali alikuwa amejitahidi kuweka wazi kanuni ambazo zitaongoza mfalme na watu, na sasa alitamani kuziwasilisha mbele yao kwa mfano wa mafunzo. Tangu utotoni, alikuwa na jukumu la kuzaliwa katika kazi ya Mungu, na katika maisha yake marefu, kitu kimoja daima kilikuwa mbele yake,--utukufu wa Mungu na uzuri mkuu wa Israeli. Hili lilikuwa inavyoonekana kwa taifa nzima, na wote sasa wanatoa ushuhuda kwa uadilifu wake na uaminifu.

Heshima iliyotolewa kwake ambaye anahitimisha kazi yake zilikuwa za thamani sana kuliko makofi na pongezi ambazo wale ambao wanaingia katika wajibu wao hupokea, na wale bado hawajajaribiwa. Mtu anaweza hata akatua mizigo yake, wakati hata adui wa ukweli wanatambua uaminifu wake. Lakini ni wangapi wa watu wetu wakuu hufunga kazi yao kwa aibu, kwa sababu wameziweka kanuni kando kwa sababu ya faida au heshima. Hamu ya kuwa maarufu, majaribu ya utajiri au raha, huwapotosha. Watu ambao wanashirikiana katika dhambi wanaweza onekana kufanikiwa; wanaweza shinda kwa sababu shughuli zao huonekana kuvikwa taji na kwa mafanikio; lakini macho ya Mungu ni juu ya wajivunaji hawa wenye kiburi. Atawalipa kulingana na kazi yao. Mafanikio makuu ya nje hayawezi leta furaha kwa wale ambao hawako katika amani na Mungu au na wao wenyewe.

Wakati mwingine inaweza kuwa muhimu kwa watumishi wa Mungu kuthibitisha tabia yake mwenyewe, na kutetea mwenendo wake, ili jina la Bwana litukuzwe, na ukweli usiaibishwe. Wale ambao wamechukuliwa kwa kuachwa au udhalimu, wafuate mfano wa Samweli, wakijiadhari wasiifanye nafsi yao kuwa maarufu, bali kudumisha heshima ya Mungu. Wale wenye kuumizwa, badala ya kukaa juu ya makosa ambayo wamepitia, waonyeshe watu jinsi wamemjeruhi Kristo katika utu wa mtumishi wake. Mioyo mingi kwa hivyo itaelekezwa kwa udhalilishaji na toba, wakati kama hisia binafsi zitaamshwa, watakuwa wagumu kama jiwe.

Isipokuwa watu waendelee kukumbatia rehema, huruma, na upendo, Shetani atahimiza kutafuta kosa, roho wa ubinafsi ambayo hutoa neema hii yenye thamani kutoka nafsini. Wale ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu na kwa kujitolea, hawapaswi kushangaa kama watawekwa kando hatimaye. Wengi wa mtu ambao Mungu amefanya kufikia matokeo makuu, ambao athari zao zimehisika mashariki na magharibi, kaskazini na kusini, mwishowe

wanatuzwa na kukataliwa au dharau ya kikatili. Kutokuwa na shukrani kihalisia ni kwa mioyo ambayo haijafanywa upya. Hakuna mtu asiye kuwa na dosari, na wengi wako tayari kupata udhuru wa kukemea, kulaumu wale ambao wamewahudumia kwa kujitolea. Wanasahao kwamba wao wenyewe wanaweza kuwa na hatia ya dhambi yenye hatia zaidi machoni pa Mungu kuliko wale ambao wanashtaki kongwe yake, kuchoka, na mtumishi mwenye kushangaa.

Inaonekana kwetu kutoendana ajabu na kuwa ajabu kwamba mtu wa wema, uaminifu na ibada ya  Samweli angewekwa kando kwa ajili ya yule ambaye alikuwa hajajaribiwa kabisa, na ambaye alikuwa karibu mgeni kwa mwenendo wa Mungu na kwa watu wake. Ila tunaona mwenendo sawa ukirudiwa mara kwa mara. Wateule wa Mungu, wale ambao wanaweza kuwa kitambo walizuiwa kwa sababu rehema, upendo, na shukurani zimetengwa kutoka kwa mioyo ya ndugu zao. Wakati watenda kazi waaminifu hawaruhusiwi tena kushikilia nafasi ya uongozi, wacha wawafundishe wale ambao watathamini juhudi zao. Wacha wafanye wema wote ambao wanaweza fanya katika kiwango chochote.  Hawajapokea mamlaka yao kutoka kwa wanadamu, bali kutoka kwa Mungu. Ni yeye ndiye amewapa kazi yao. Kama wamefungiwa kutoka kwa njia zingine zote za umuhimu, wanaweza omba. Wamemthibitisha Bwana tena na tena; wanauzoefu wa neno lake, na wanaweza dai ahadi zake. Mungu husikia maombi yao.

Tunapaswa kujifunza kuheshimu wale ambao Mungu anaheshimu. Wale ambao wamefanya kazi kwa muda mrefu na kwa kujitolea katika kazi yake wanafaa kuheshimiwa daima na kuhurumiwa, hata ikiwa wazi kwamba hawawezi tenda kazi ambayo wakati mmoja waliweza, au, kwamba wakati mwingine hupotea katika hukumu. Bila ya kujali kasoro zao, watu hawa hasa wanaweza kuwa muhimu sana katika kazi ya Mungu, kuliko wale ambao wanawakosoa na kuwakataa. Wote wanakasoro katika tabia. Wote wanahitaji msaada wa Mungu kila saa, au wataanguka kwa kuamua.

Samweli alisoma mbele ya Israeli matukio ya kuongoza katika historia yao iliyopita, udhihirisho wa ajabu wa nguvu ya uungu, na ushahidi wa fadhila yake katika kuwaanzisha kuwa watu wateule. Aliwakumbusha uovu wao katika kuondoka kwa Mungu, na kutafuta kuiga mfano wa mataifa yaliyowazunguka; aliashiria hukumu ambazo zilikuwa zimepatilizwa juu yao kwa dhambi zao, na ukombozi wa neema ambao toba yao ilikuwa imepokea. **Majanga yao yote yalikuwa yameletwa na uasi wao dhidi ya Mungu. Mafanikio yao yalikuwa yamepatikana kwa kutii. Ila walipotishiwa na adui zao, hawakumfanya**

**Mungu imani yao, bali walidai mfalme wa kuongoza majeshi yao. Samweli alikuwa amejaribu kuwahimiza watumainie Msaidizi Mtakatifu, na hata kujitolea kuwaongoza katika vita yeye mwenyewe; lakini walikuwa wamekataa kwa ujeuri pendekezo lake.**

Sasa Bwana alikuwa amewatimizia hitaji lao, na akaweka mfalme juu yao; ingawa mafanikio yao bado yangetegemea utiifu wao kwa Mungu. Bila ya kujali dhambi zao, Mungu angewasamehe na kuwabariki kama kuanzia wakati huo wangeonyesha toba ya kweli na uaminifu. Lakini," akasema nabii, "Bali msipoisikia sauti ya Bwana, mkiiasi amri ya Bwana, ndipo mkono wa Bwana utakuwa juu yenu, kama ulivyokuwa juu ya baba zenu."

Kama dhibitisho la ukweli wa maneno yake, na pia kama ushahidi wa hasira ya Bwana, **Samweli aliita radi na mvua kutoka mbinguni. Ukiwa wakati wa kuvuna ngano, wakati ambao anga ni tulivu na pole, watu waliogopa sana dhihirisho hili, na wakaungama dhambi zao, wakaitikia maombi ya nabii kwa niaba yao. Sasa waliona kuwa Mungu alikuwa amemheshimu sana mtu ambaye walikataa**; na walihisi wakati huo kwamba walikuwa wamefanya kosa kubwa kwa kupinga mpangilio wenye hekima wa Bwana.

**Samweli hakuwaacha watu katika hali ya kutamausha. Alijua kwamba hili lingezuia jitihada zake zote za maisha bora. Wangemuona Mungu kama asiyesamehe na mkatili, na kwa hivyo wangewekwa wazi kwa majaribu mbalimbali. Hiyo sio tabia ya Mungu wetu mwenye rehema**. Ni mwenye huruma na kusamehe, daima yuko tayari na mwenye hamu ya kuonyesha upendeleo kwa watu wake watakapoisikia na kuitii sauti yake. Alisema nabii, "Msiogope; ni kweli mmeutenda uovu huu wote; lakini msigeuke na kuacha kumfuata Bwana, bali mtumikieni Bwana kwa mioyo yenu yote; Wala msigeuke upande, maana, kufuata vitu vya ubatili visivyoweza kusaidia wala kuokoa, kwa kuwa havifai kitu. Maana Bwana hatawaacha watu wake." Samweli pia aliwahakikishia watu kuendelea kwake kuomba kwa niaba yao, na pia huduma yake kwa hakimu na mwalimu. Alimalizia hotuba yake kwa onyo, "Lakini kama mkiendelea kutenda mabaya, mtaangamia, ninyi na mfalme wenu pia."

Maisha ya Samweli ya utakatifu na kujitolea kwa kujikana nafsi kwa kazi ya Mungu, yenyewe yalikuwa kemeo la daima kwa Waschemu, makuhani wenye kujipenda, na wazee na wenye kiburi, umati wa kutamani wa Israeli. Ingawa hakuchukua fahari yoyote na hakuhimiza onyesho lolote, kazi yake ilikuwa na muhuri wa Mbinguni. **Aliheshimiwa na Mkombozi wa ulimwengu, ambaye kwa uongozi wake alitawala taifa la Waebrania. Lakini watu walichoshwa na**

**ucha Mungu wake na ibada, wakadharau utawala wake mnyenyekevu, na wakamkataa na kutaka mtu atakaye watawala kama mfalme.**

**Katika tabia ya Samweli tunaona ukiakisiwa mfano wa Kristo. Usafi usiokuwa na doa wa maisha ya Mkombozi wetu ulimkasirisha Shetani**. Maisha hayo yalikuwa nuru ya ulimwengu, na yalidhihirisha uharibifu uliofichika katika mioyo ya wanadamu. **Ni utakatifu wa Kristo ndio ulichochea shauku ya ukatili wa profesa wa fasiki ya uungu dhidi yake.**

Kristo alikuja sio kwa utajiri na heshima ya dunia, ila kazi ambaye alitenda ilimuonyesha kuwa na uwezo mkuu sana kuliko mwana yeyote wa mfalme wa kibinadamu. Wayahudi walitafuta Masihi ambaye atavunja nira ya mnyanyasaji, ila walipenda dhambi ambazo zilikuwa zimefungwa katika shingo zao, hawangestahimili kukemewa kwa ushupavu na Kristo kwa uovu wao. Upendo katika tabia ambayo ukarimu, usafi, na utakatifu zilitawala kwa ukuu, ambao haukuruhusu chuki yoyote isipokuwa ya dhambi, waliudharau. Kama Kristo angezifunika dhambi zao na kushukuru uungu wao, wangemkubali kama mfalme. Walimchukia kwa sababu alipigana vita na kiburi, unyanyasaji, tamaa, na unafiki.

Hivyo ndivyo imekuwa katika kila kizazi cha ulimwengu. Nuru kutoka Mbinguni huleta hukumu juu ya wote ambao hukataa kutembea kwayo. Ni jukumu la kila Mkristo kudumisha heshima ya Mungu kwa kujikana nafsi, maisha bila doa, na kukemea dhambi katika mitindo yake yote kwa ushupavu. Shetani atafanya jitihada kuu kuwafagia kutoka ulimwenguni wale ambao wanadumisha usafi na ucha Mungu. Lakini kwa nguvu mno kuliko anavyowakaribia waaminio, mioyo yenye kuamini, na kupima silaha na mkuu wa giza. Katika kila kipindi kumekuwa na watu waaminifu wanaosimama kama mashahidi wa Mungu duniani. Wakati huu wa sasa ni wakati wa giza na unyonge kwa makanisa; lakini hili ni kwa sababu hawajaunganishwa kwa Kristo. Kupooza kwa maadili miongoni mwa wanaodai kuwa Wakristo hakupaswi kuwa. Wanaweza kuwa na nguvu za ujana wa daima, kama wataweka kando sanamu zao, na kumtumikia Mungu kwa moyo mkamilifu.

“Yeyote anayetaka kuishi maisha ya utauwa ndani ya Kristo Yesu atateswa.” Moyo halisi sasa uko katika upinzani kwa nguvu, kama katika siku za Samweli au za Kristo. Wanapokemewa kwa mfano wa wale wanachukia dhambi, wanafiki watakuwa mawakala wa Shetani wa kunyanyasa na kutesa waaminifu. “Lakini,” asema mtume, “Ni nani atakayewadhuru mkiwa wenye bidii katika kutenda mema?” Hao kwa imani wamepokelewa katika familia ya Mungu; watakuwa zaidi ya washindi kupitia kwake aliyewapenda.

# 4. Dhabihu Iliyokataliwa.

Sauli alipokwisha vishwa taji Gilgali, taifa lilionekana kutojulikana kwa uungaji mkono kwake, na alihisi kuwa enzi yake ilikuwa imara na dhabiti. Sasa aliwachilia nyumbani mwao jeshi kubwa ambalo lilikuwa limezuka katika wito wake wa kushinda Waamoni, akibakisha tu watu elfu mbili watakaowekwa chini ya amri yake katika Mikmashi, na elfu moja wa kumshughulikia mwanawe Yonathani katika Gibea ya Benyamini.

Akijawa na heshima za ushindi wa hivi karibuni, Sauli alikuwa ameelekea kulegeza jitihada zake. Alipendelea kufurahia raha na fahari ya kifalme kuliko taabu, kubahatisha, na hatari za uwanja wa vita. Hapa kulikuwa na kosa kubwa. **Ingawa jeshi lake lilikuwa limejawa na tumaini na ujasiri, angeenda mbele mara moja na kufanya vita dhidi ya adui wengine wa Israeli. Kwa kupuuza kufanya hili, alipoteza fursa ya kupiga pigo la kuwaambia kwa ajili ya heshima ya Mungu na uhuru wa taifa.[7]**

Wakati huo huo jirani zao wapendao vita, Wafilisti, walikuwa kazini. Baada ya kushindwa Ebneza, bado walikuwa wamebakisha umiliki wa baadhi ya milima kati nchi ya Israeli; na sasa wakitumia fursa ya hali ya kukosa mpango katika taifa la Waebrania, kutokana na athari ya mabadiliko ya utawala, adui hawa wenye nguvu walikuwa wamejiendeleza katika kila moyo wa taifa. Ila walijawa na hofu kwa kushindwa kwa Waamoni wakali na wakatili, na kama wangevamiwa kwa ujasiri na nguvu sawa, wakati huo wangeweza kushindwa.

Kwa vifaa, silaha, na mali, Wafilisti walikuwa na manufaa kubwa zaidi ya Israeli. Wakati wa kipindi kirefu cha utawala wao wa ukandamizaji, walikuwa wamejitahidi kuimarisha nguvu zao, kwa kuwazuia Waisraeli kushiriki katika biashara ya kufua vyuma, wasije wakatengeneza silaha za vita. Katika hitimisho ya amani, bado walikuwa wamehifadhi biashara mikononi mwao wenyewe, Waebrania wakitegemea ngome ya Wafilisti kwa kuwa kazi kama hiyo ilihitaji kufanywa. **Kama watu wa Israeli wangekuwa na nguvu na mtazamo sahihi, wangeweza, wakati wa kipindi kirefu cha amani, kupata huduma za mafundi**

[7] Inatia msomaji katika majaribu kufikiria kwamba Mungu anahimiza kuwepo kwa vita lakini sivyo. Waisraeli wamemkataa Mungu na wanaishi katika Agano la Kale. Njia ya kupona inahusisha kupitia katika majaribu walioanzisha wenyewe. Mungu hawaachi Waisraeli hata ingawa wamemuacha. Bado anasaidia wanawe waliopotoka na kuwahimiza kurejea mahali ambapo walimuacha.

**wenye ujuzi, na kujipatia silaha za vita**.[8] Lakini pendo la raha, na roho aliyekithiri ikitiwa na muda mrefu wa ukandamizwaji, iliwathibiti. Hivyo walikuwa wameteseka hata vifaa vyao vya kilimo vikawa butu, na hakuna yeyote miongoni wa Israeli, isipokuwa Sauli na mwanawe Yonathani, alikuwa na mkuki au upanga.

Haikuwahi fanyika hadi mwaka wa pili wa utawala wa Sauli kwamba jaribio lilifanywa la kuwashinda Wafilisti. Pigo la kwanza lilitoka kwa Yonathani, ambaye kwa amri kutoka kwa baba yake alivamia na kuwashinda ngome yao ya Geba. Wafilisti walivurugika sana kwa ushindi, na walijitayarisha kuvamia Israeli kwa haraka.

Sauli sasa aliamshwa na hitaji la tendo la mara moja. Alifanya vita kutangazwa kwa sauti ya tarumbeta katika nchi yote, na pia akatoa wito akiwaita watu wote wa vita, ikiwemo makabila yaliyoizunguka Yordani, kukusanyika mara moja Gilgali. Wito huu ulitiiwa.

Wafilisti walikuwa wamekusanya jeshi kubwa katika Mikmashi—"magari thelathini elfu, na wapanda farasi sita elfu, na watu kama mchanga ulio ufuoni mwa bahari kwa wingi wao." Wakati Waebrania walisikia nguvu na hesabu ya wapinzani wao, na kisha wakazingatia hali ya kutoweza kujikinga, walijawa na hofu na kukata tamaa. Kila siku jeshi la Sauli lilififia, kadri makundi ya watu walikimbia kujificha katika mapango, vichaka, na mashimo; na wengine hata walikimbilia Yordani, katika mji wa Gadi na Gileadi. Wale ambao walibakia "wakamfuata wakitetemeka."

Sasa kiburi na ujasiri wa Israeli katika mfalme wao zilikuwa wapi, waliyedai, kama walivyokuwa wametangaza, "ili sisi nasi tufanane na mataifa yote; tena ili mfalme wetu atuamue, tena atoke mbele yetu na kutupigia vita vyetu'? Ole, ni jinsi gani hawana maana kabisa wote ambao matumaini yao yote yako kwa fahari au kiburi cha mwanadamu!

Samweli alikuwa ameteua kukutana na mfalme Gilgali, kule ili "kutoa sadaka ya kuteketezwa, na kuona kile ambacho angefanya." Nabii hakufika kwa wakati ambao ulinenwa, na Sauli alipoona hatari ikiongezeka, na mioyo ya watu ikijawa na hofu, alikosa uvumilivu. Badala ya kufikiria ombi, na kunyenyekeza

---

[8] Tena muktadha ni muhimu. Waisraeli wanawekwa mahali ambapo lazima waende vitani kwa sababu walitaka kuwa kama mataifa mengine. Mpango asilia wa Mungu ulikuwa kufukuza mataifa kwa mavu (Kut23:28) badala ya kuchukua nchi kwa vita. (PP 392)

nafsi yake kwa Mungu, aliamua kufanya kitu yeye mwenyewe ili kutatua magumu ya hali.

Hapa ndipo watu wengi wameangukia, na wanaendelea kuanguka. Hawangojei kwa uvumilivu Bwana awatendee. Wanatamani kuwa kazini, na kama Mungu hawapi kitu cha kufanya, wanajiingiza kufanya hata kile ambacho amekataa. Bwana alikuwa amemtia kizuizini mtumishi wake ili kujaribu imani na utiifu wa mfalme. Sauli hakupita jaribio. Mungu alikuwa ameahidi kuwa naye, kama atatii. Angeamini ahadi yake, na asubiri kwa uvumilivu maagizo na maelekezo takatifu. Lakini akidhani kwamba lazima jambo litekelezwe mara moja ili kuwatia watu ujasiri, aliwaamuru kuleta mbele wahadhiriwa wao kwa kafara, na kisha kwa kujikinai alichukua pahala pa kuhani, na yeye mwenyewe akawatoa kafara kwenye madhabahu. Tendo hili lilikuwa kwa uwazi ukiukaji wa agizo takatifu kwamba wale tu ambao wanapaswa kutoa kafara ni wale ambao walikuwa wamewekwa wakfu kwa kazi hiyo. **Zaidi ya hayo, hali ya umma ya kitendo, na vile vile cheo cha juu cha mkosaji, viliongezea pakubwa kwa athari mbaya ya mfano wake, na ikaweka adhabu ya haraka na lazima kuwa muhimu**.[9]

Pindi tu Sauli alipokuwa amemaliza kutoka sadaka ya dhabihu, alisikia kukaribia kwa Samweli, na akaenda kumlaki. Na ingawa alisalimiwa kwa maonyesho ya heshima na upendo, nabii alifahamu kuwa yote hayakuwa sawa. Katika mwitikio alichunguza, "Umefanya nini?" Sauli alijaribu kutoa udhuru kwa mwendo wake mwenyewe, kwa kuonyesha tisho la watu na hatari ya uvamizi wa mara moja kutoka kwa Wafilisti. Lakini nabii aliwarudishia jibu kali na makini, -- "Umefanya upumbavu; hukuishika amri ya Bwana, Mungu wako, aliyokuamuru; kwa maana Bwana angaliufanya ufalme wako kuwa imara juu ya Israeli milele. Lakini sasa ufalme wako hautadumu; Bwana amejitafutia mtu aupendezaye moyo wake, naye Bwana amemwamuru yeye kuwa mkuu juu ya watu wake, kwa sababu wewe hukulishika neno lile Bwana alilokuamuru."

Uovu wa Sauli ulimdhibitisha kutofaa kukabidhiwa majukumu takatifu. Ambaye alikuwa na heshima ndogo kwa mahitaji ya Mungu, hangekuwa kiongozi mwenye hekima au salama kwa taifa. Kama angeshinda kwa uvumilivu jaribio takatifu, taji ingethibitishwa kwake na nyumba yake. Kwa hakika, Samweli alikuwa amekuja Gilgali kwa kusudi hili. Lakini Sauli alikuwa amepimwa kwenye mizani, na akaonekana kupungukiwa. Lazima aondolewe

[9] Kanuni hii itakuwa muhimu baadaye tutakapoangazia kisa cha Agagi.

ili kutengeneza njia kwa yule ambaye ataheshimu kitakatifu heshimu na mamlaka takatifu.

Mungu mwenye hekima yote alikuwa ameona awali matukio haya, ila udhalilishaji wa tishio wa Sauli ulilipwa tu kwa dhambi na upumbavu wake mwenyewe. Mungu alikuwa amempa fadhila kuu ya kukuza tabia yake. **Roho Mtakatifu alikuwa amangaza ufahamu wake, akimpa mitazamo wazi ya tabia na mahitaji takatifu, na ya wajibu wake mwenyewe. Yote haya yalifanya dhambi yake kuhuzunisha Zaidi.**

Kama Sauli angekumbatia nuru ambayo Kristo alikuwa amempa, angeamini kwa kiasi kidogo matendo ya ibada za kidini, na angehisi kwa kina zaidi umuhimu wa kunyenyekeza moyo wake mbele za Mungu. Msukumo ungeongozwa na mantiki, na kuadhibiwa na kutakaswa na dhamira. **Lakini ni vigumu kwa mtu ambaya ambaye tabia zake ni imara, kufuta kile ambacho amejifunza kwa miaka mingi**. Neema takatifu pekee inaweza tekeleza badiliko hili.

Katika kutenda kwa uaminifu mapenzi ya Mungu, nguvu zote za akili, hisia zote za moyo, zitatiwa kwa kazi yao bora zaidi, safi kabisa, tendo la furaha. Fadhila za mkristo ni kuu zaidi, na mabadiliko ambayo yatafanywa na Roho Mtakatifu ni makuu, ili sasa watu wenye asili ya dhambi waweze kuwa wana wa Mungu. Uwezo wa akili na hisia za kiroho, hazina za kumbukumbu na utarajiaji wa tumaini, pia vile vile zitatakaswa na roho wa Kristo, na kuwekwa wakfu kwa huduma yake. Maisha ya mwanafunzi wa Kristo huanzwa kwa imani na kuendelezwa kwa utiifu.

## 5. Ushindi Wa Mikmashi.

Nguvu na ujuzi wa kijeshi ulioonyeshwa na Sauli katika kumshinda Jabesh-gileadi ziliinuliwa na taifa nzima. **Katika shauku yao watu walisahau kwamba alikuwa tu wakala ambaye Bwana alikuwa amemfanya kwa ukombozi wao. Na ingawa mwanzo mfalme aliweka utukufu kwa Mungu, baadaye alichukua heshima juu yake**. Alipoitwa kwenye kiti cha mfalme mara ya kwanza, alikuwa mnyenyekevu na mwaminifu; lakini mafanikio yalimfanya kuwa na ujasiri binafsi, na muda mrefu sasa alikuwa na hatia ya dhulma na kufuru, katika kutoa dhabihu ambayo hakuruhusiwa kule Gilgali.

Ujasiri sawa wa kipofu ulimpelekea kukataa ujumbe wa Samweli wa maonyo. Sauli alimtambua Samweli kuwa nabii aliyetumwa kutoka kwa

Mungu. Kwa hivyo alipaswa kukubali maonyo, ingawaje yeye mwenyewe hangeona kwamba alikuwa ametenda dhambi. Mwenendo kama huo, kuonyesha utayari wa kukosolewa, ungeenda zaidi na kumrejesha katika fadhila za Mungu. **Lakini Sauli alijitahidi kutetea mwenendo wake mwenyewe, na kumlaumu nabii, badala ya kujilaumu mwenyewe.**

Kuna wengi leo ambao wanafuata mwenendo sawa. Kama Sauli, wamepofushwa wasione makosa yao. Wakati Bwana anatafuta kuwakosoa, wanapokea maonyo kama tusi, na kuona kasoro kwa yule ambaye analeta ujumbe takatifu.

Kama Sauli angekuwa tayari kuona na kutubu kosa lake, hisia hizi chungu zingethibitisha kuwa usalama wa siku za usoni. Baadaye angeepuka makosa ambayo yalihitaji maonyo takatifu. Lakini kuhisi kwamba alikuwa amelaumiwa bila haki, bila shaka, angekuwa katika uwezekano wa kurudia tena kosa hilo.

Bwana angetaka watu wake, katika hali zote, wadhihirishe imani thabiti kwake. Ingawaje hatuwezi elewa wakati wote matendo ya huduma yake, tunapaswa kusubiri kwa uvumilivu na unyenyekevu hadi itakapompendeza kutuangazia. Tunapaswa kujihadhari na kuchukua majukumu ambayo Mungu hajatupa mamlaka ya kuyatekeleza. Watu mara nyingi wanakuwa na makadirio makubwa zaidi ya tabia au uwezo wao wenyewe. Wanaweza hisi kuwa na uwezo wa kufanya kazi muhimu zaidi, wakati ambao Mungu anaona kwamba hawajaandaliwa kufanya vyema wajibu mdogo kabisa na wa unyenyekevu kabisa.

Sauli alikuwa katika upinzani na Mungu, na bado hakuwa tayari kunyenyekeza moyo wake katika kitubio. Alitamani kuzua mipango fulani ya kutweka thabiti zaidi mamlaka yake ya kifalme, na vile vile kufufua ujasiri wa watu. Kile alikosa katika ucha mungu wa kweli, angejitahidi kutengeneza madhara na maonyesho. **Sauli alifahamu historia ya kutisha ya kushindwa kwa Israeli wakati ambao sanduku la Bwana lililetwa kambini na Hophini na Phinehasi; ila, akijua haya yote, aliamua kutumana sanduku takatifu na kuhani wa kulihudumia**.

Kwa roho wa kujiadhimisha anaingia katika kutimiza mipango yake. Alitumainia kuhuisha mioyo ya Israeli kwa nguvu mbichi, kukusanya upya jeshi lake lililotapakaa, na kuwashinda Wafilisti. Sasa atagawa kwa uwepo wa Samweli na uungaji mkono, na kwa hivyo kujiweka huru kutoka kwa kukosolewa kusichokubalika na maonyo makali ya nabii. **Anahisi kwamba Samweli hathamini kwa usahihi cheo na mamlaka ya mfalme, na kwa hivyo**

**hamhudumii kwa heshima sahihi**. Anatarajia kwamba Ahiahi kuhani atanyenyekezwa na heshima za kifalme, na atakubaliana na maneno ya mfalme kama mkuu.

Roho Mtakatifu alikuwa ametolewa kwa Sauli kuangazia ufahamu wake na kupunguza ugumu wa moyo wake. Alikuwa amepokea kwa uaminifu maagizo na maonyo kutoka kwa nabii wa Mungu. Ila upotovu ni mkuu kiasi gani! Historia ya mfalme wa kwanza wa Israeli inawasilisha mfano wa kuhuzunisha wa tabia mbaya za awali. **Katika ujana wake, Sauli hakumcha na kumpenda Mungu; na moyo huo wa hasira, ambao haukufunzwa kunyenyekea mapema, daima ulikuwa tayari kuasi dhidi ya mamlaka takatifu**.

Funzo ni ambalo wote watafanya vyema kulitafakari. Watu hawawezi kwa miaka kunyanyasa nguvu bora zaidi ambayo Mungu amewapa kwa ajili ya huduma yake, na kisha, wanapochagua kubadilika, wapate nguvu hii ikiwa bichi na huru kwa mwendo kinyume kabisa. Wale ambao katika maisha ya awali wanakumbatia mahusiano takatifu ya mamlaka ya Mungu, na wale ambao wanatekeleza kwa imani wajibu wa nafasi zao, wataandaliwa kwa huduma za juu katika miaka ya baadaye. Kama tutashinda katika vita vya maisha, lazima tuzingatie ushauri wa hekima isiyo na mwisho, mwanzo na mwisho na kila wakati.

Jitihada za Sauli za kuhamasisha watu na tumaini na ujasiri zilithibitisha kutokuwa kitu. Akipata jeshi lake limepunguzwa hadi watu mia sita, aliondoka Gilgali, na akastaafu kwa ngome ya Gebea, ambayo ilikuwa imenyakuliwa karibuni kutoka kwa Wafilisti. Ngome hii ilikuwa upanda wa kusini wa bonde ndefu la muinuko au umio, maili chache kaskazini mwa tovuti ya Jerusalemu. Upande wa kaskazini mwa bode hilo, Mikmashi, Jeshi la Wafilisti lilikita kambi, wakati ambao makundi ya majeshi yaliondoka kwa pande tofauti kuangamiza inchi.

Kwa upande mmoja kulikuwa na kundi la watu wachache ambao karibu hawakuwa wamejihami kwa silaha, kwa upande mwingi, hesabu kubwa sana ya majeshi yaliyojipanga vizuri, na elfu thelathani za magari ya farasi ya chuma. Ni ajabu gani kwamba mioyo ya watu wa Israeli ilijawa na hofu! Mungu alikuwa ameruhusu mambo hivyo yaletwe kwenye mgogoro, ili aweze kukemea upotovu wa Sauli, na kufundisha watu wake somo la uvumilivu na imani.

**Yonathani, mwana wa mfalme, mtu ambaye alimcha Mungu, aliteuliwa kama chombo cha kuokoa Israeli**.[10] Akiongozwa na msukumo takatifu, alipendekeza kwa mbeba silaha wake kwamba wafanye ushambulizi wa siri dhidi ya kambi ya adui zao. “Inaweza kuwa,” alisihi, “yamkini Bwana atatutendea kazi; kwa maana hakuna la kumzuia Bwana asiokoe, kwamba ni kwa wengi au kwamba ni kwa wachache.”

Mbeba silaha, mtu wa imani na maombi, alihimiza mtindo huo, na pamoja wakaondoka kutoka kwa kambi ya Israeli, kisiri, lengo lao lisije likapingwa kama la kiburi. Kwa maombi ya kina kwa Uongozi wa baba zao, walikubaliana kuhusu ishara ambayo wataamua jinsi wataendelea. Kisha wakipita katika umio wakitenganisha jeshi hizo mbili, na ambazo hapa waliweka nusu maili ya upana, kimya kimya walifuata njia yao, chini ya kivuli cha jabali, na kwa kiasi wakifichwa na kifusi na safu za bonde. Wakikaribia ngome ya Wafilisti, walijiwekwa wazi kwa mtazamo wa adui zao ambao walisema kwa mshangao, “Kumbe! Wale Waebrania watoka katika mashimo walimojificha,” kisha wakawaambia, “Haya! Ninyi, pandeni juu hapa tulipo, na sisi tutawaonyesha jambo,” kumaanisha wangewaadhibu Waisraeli hao wawili kwa kuthubutu.

Changamoto hii ilikuwa ishara ambayo Yonathani na rafiki yake awali walikuwa wamekubaliana kuipokea kama ushahidi kwamba Bwana atafanikisha shughuli zao. Wakipita sasa machoni mwa Wafilisti, na kuchagua njia ya siri na ngumu, mashujaa walifika kwenye kilele cha jabali kabla ya kuonekana isiyofikika, na kwa hivyo kutokuwa na ulinzi dhabiti. Kwa hivyo walipenya kambi ya adui, na kuwaua waangalizi, ambao walilemewa kwa mshangao na hofu kiasi cha kutotoa upinzani.

Jeshi nzima lilififishwa na bumbuazi, ambayo iliongezwa na tetemeko la ardhi likitendeka kwa muujiza wakati huo huo. Wafilisti walidhani kuwa jeshi kubwa lilikuwa juu yao, na katika kuchanganyikiwa kwao wakaanza kuuana wenyewe.

Upesi kelele za vita zilisikika katika kambi ya Israeli. Baada ya kuulizia ilipatikana kwamba hakuna ambaye hakuwepo ila Yonathani na mbeba silaha wake. **Sauli mwanzo alitamani kumuuliza Bwana kama shambulizi lifanywe dhidi ya Wafilisti; lakini mkanganyiko miongoni mwao uliongezeka dhahiri, moyo wake usiokuwa na subira haungechelewesha kijito.** Akipanga jeshi lake

[10] Haivutii zaidi kutambua kwamba badaa ya kushinda vita ndio Sauli aliamua kumuua Yonathani, mwanawe. Badala ya kunyenyekea na kutubu, alitamani kumuua yule ambaye Mungu alipendelea kusaidia Waisraeli.

ndogo, alipanda juu dhidi ya adui. Waebrania ambao walikuwa wameachwa kwa Wafilisti, sasa walijiunga na watu wenzao; hesabu kubwa pia ilitoka mafichoni mwao, na Wafilisti walipokuwa wakikimbia, wakishindwa, jeshi la Sauli lilitenda maangamizi ya kutisha juu ya wakimbizi.

## 6. Kiapo cha Haraka cha Mfalme Sauli.

Sauli alipowatazama Wafilisti wakikimbia kwa hofu kutoka Mikmashi, aliamua kufanya kikubwa cha manufaa yake. Ili kuepuka kuchelewa kusiokuwa na maana, aliwazuia wafuasi kula chakula kwa siku nzima, akilazimisha amri yake kwa laana makini, "Na alaaniwe mtu awaye yote alaye chakula cho chote hata jioni, nipate kujilipiza kisasi juu ya adui zangu."

Mfalme angewaonya vyema askari wake wasipoteze muda katika kula kwa maeneo ya adui zao waliyoteka; lakini **kuwanyima chakula siku nzima ni ukosefu wa hekima uliokithiri**. Kujizuia kwa muda mrefu kuliwafanya wadhaifu na wachovu wakati hasa ambao walipaswa kuwa na nguvu na ujasiri wa kusukuma vita dhidi ya adui. Na kisha kuthibitisha marufuku haya yasiyo kuwa na uzingatifu kwa kiapo kulimwonyesha Sauli kuwa mweye kasi na wakidunia. **Mwenendo kama huo haungesababishwa na jitihada za utukufu wa Mungu**. Mfalme alitangaza lengo lake kuwa, sio "ili bwana apate kujilipiza kisasi juu ya adui zake," kama tu "ili nipate kujilipiza kisasi juu ya adui zangu." Ingawa ukweli ulikuwa kwamba, Sauli hakuwa na sehemu hasa katika vita; ushindi ulikuwa umepatikana bila maarifa au ushirikiano wake.

Wakihofu hasira ya mfalme, askari walijizuia kutoka kwa kushiriki maangamizi ya adui zao, na hata kwa kula asali ya mwito ambayo ilipatikana kwa wingi walipokuwa wakipitia mwituni. Lakini Yonathani alipuuza marufuku ya baba yake, na bila kujua akaasi kwa kuchovya asali kidogo.

Jioni, wakiwa njaa, na kufifia kwa kazi, wengi wa watu walichinja ng'ombe waliokuwa wamechukua kwa haraka, na wakala nyama pamoja na damu, kinyume na sheria. Hivyo ndivyo ukali na ukosefu wa busara wa Sauli ulipelekea kwa kuvunjwa kwa sheria takatifu. Hata hivyo wakati ambao mfalme alipojua kilichokuwa kikiendelea, aliingiza mamlaka yake, na akaagiza kwamba kafara kwanza itolewe kwa Bwana, na kisha wanyama wachinjwe vizuri na damu iondolewe, kama vile sheria ya Musa iliamuru.

Watu walipokuwa wameridhisha shauku yao, Sauli alipendekeza kuendeleza azma yake usiku huo; lakini kuhani alipendekeza kwamba ni jambo

la busara kwanza kuuliza ushauri kutoka kwa Mungu. Hili lilifanywa kwa njia ya kawaida; lakini hakuna jibu ambalo lilikuja. Kuhusiana na kimya hiki kama ishara ya hasira ya Bwana, Sauli aliamua kugundua kisababishi. **Kama angetambua kwa usahihi uovu wa mwenendo wake mwenyewe, angehitimisha kwamba yeye ndiye alikuwa na hatia. Lakini kwa kukosa kutambua hili, alitoa amri kwamba suala hili liamuliwe kwa kura**. "Karibieni hapa, enyi wakuu wote wa watu; mjue na kuona dhambi hii ya leo imekuwa katika kosa gani. Kwa maana, aishivyo Bwana, awaokoaye Israeli, ijapokuwa i katika Yonathani, mwanangu, kufa atakufa." Watu walisikiliza kwa ukimya, mioyo yao ilichangamshwa kwa hofu, walipoona roho ya kasi ya mfalme wao wenye hasira.

Tena mfalme aliamuru, "Ninyi mtakuwa upande mmoja, na mimi na mwanangu Yonathani tutakuwa upande wa pili." **Kura ilipigwa; ikamwangukia Sauli na Yonathani. Ikapigwa tena, na Yonathani akachukuliwa**.[11] Bwana alipendezwa kwamba mwendo wa Yonathani uletwe katika nuru, kudhihirisha kikamilifu zaidi roho ya Sauli. Hivyo watu waongozwe kuona kosa lao kuu katika kukataa utawala ambao Bwana alikuwa amewapa. Walikuwa wamembadilisha nabii mcha Mungu ambaye maombi yake yalikuwa yameleta mibaraka, na mfalme ambaye katika jitihada yake ya kipofu alikuwa ameomba laana juu yao.

Kura ilipomwangukia Yonathani, mfalme alitaka kujua kwa ukali mwingi, "Niambie umefanya nini?" Yonathani alijibu kwa uwazi, akikubali kitendo, na akiomba msamaha kwa adhabu angafu. Sasa hatimaye tunaweza tarajia Sauli kuona na kulaani ujinga wake katika kufanya kiapo cha haraka. Sasa, hakika, upendo wa baba utazuka kuwa mkuu kwa mamlaka ya kifalme. Lakini hapana; Sauli alitamani watu wake waone kwamba haki ya mfalme ni kubwa kuliko upendo wa baba. Hakuwa ameshiriki heshima ya ushindi; lakini sasa alitarajia kupata heshima kwa jitihada yake ya kudumisha utakatifu wa kiapo chake. **Hata katika kutoa kafara ya mwanawe, angevutia kwa anaowatawala ukweli kwamba mamlaka ya kifalme lazima yadumishwe.[12] Ni ya umuhimu sana**

[11] Inavutia kugundua jinsi kura ilimwangukia Yonathani ikiakisi tamaa ya Sauli kuepuka shtaka ya tendo ovu. Mungu aliruhusu kura imwangukie Yonathani ili kwamba tabia ya mfalme iweze kudhihirishwa. Baba wa kweli atachukua jukumu katika suala hili, lakini sio Sauli mwenye moyo mgumu.

[12]Hivi ndivyo watu hufikiria kuwa Mungu huilinda enzi yake kwa kuleta kio kwa wengine ili kuonyesha kuwa hana mzaha.

**maneno ambayo yalitoka katika midomo ya baba,--"Mungu anifanyie hivi, na kuzidi; kwa kuwa hakika utakufa, Yonathani**."

Pale Gilgali, lakini muda mfupi awali, Sauli alikuwa amejiweka kuongoza kama kuhani, uasi wa moja kwa moja wa amri ya Mungu. Alipokaripiwa na Samweli, alikuwa amehalalisha kitendo chake kwa ukaidi. Sasa, kwa tuhuma wazi za dhambi katika lingine--kabla ya kura kupigwa—alikuwa ameapa kwamba hakika mkosaji atauawa; bila kuzingatia kuwa kosa linaweza kuwa dhambi ya kutojua, la kusafishwa kwa kafara ya dhambi, badala ya kosa la makusudi la kuadhibiwa kwa kifo.

Wakati mkosaji amegunduliwa, na inajulikana kuwa uhalifu wake tu ni ukiukaji bila kujua wa mahitaji yasiyokuwa na maana, mfalme na baba kwa baridi anamhukumu mwanawe kifo. **Ni tofauti namna gani kati ya ujasiri ambao Sauli mwenyewe anakiuka sheria ya Mungu na ananajisi maonyo, na ukatili mkali unaodhihirishwa naye kwa yule ambaye Mungu alikuwa ameheshimu![13]**

Watu walikataa kuruhusu hukumu hii dhalimu itekelezwe. Waliona ambapo hatia ilitoka; kwamba Sauli mwenyewe ndiye Mungu alikuwa anakemea. Kutotii hasira ya mfalme, walitangaza wazi, "Je! Atakufa Yonathani, ambaye ndiye aliyeufanya huo wokovu mkuu katika Israeli? Hasha! Aishivyo Bwana, hautaanguka chini hata unywele mmoja wa kichwa chake; kwa maana ametenda kazi pamoja na Mungu leo." Uamuzi wa cheo! Watu wenye hekima na jasiri! Mfalme mwenye kiburi alithubutu kutopuuza uamuzi huu wa jumla, na uzima wa Yonathani ulihifadhiwa.

**Sauli angehisi kwamba mwanawe alipendelewa kumliko, na watu na Bwana pia**.[14] **Kukombolewa kwa Yonathani kulikuwa onyo kali kwa kasi ya mfalme. Alihisi kibuhuti, kwamba laana zake zingeanguka juu ya kichwa chake mwenyewe.** Hakuendelea kwa muda kupigana na Wafilisti, bali alirudi nyumbani kwake, mwenye hasira na kutoridhika.

---

[13] Na kwa hivyo amedhihirishwa mtu asilia katika utukufu wake wote.

[14] Tabia ya Sauli ilikuwa kiasi ya kwamba alipoamini wengine walipendelewa mbele zake, wivu wake uligeuka hasira na akawa muuaji. Hili ndilo alitenda hasa. 1 Sam 14:47 Basi Sauli alipokwisha kuutwaa ufalme juu ya Israeli, alipigana na adui zake zote pande zote, juu ya Moabu, na juu ya wana wa Amoni, na juu ya Edomu, na juu ya wafalme wa Soba, na juu ya Wafilisti; na po pote alipogeukia, akawashinda.

Wale ambao wako tayari zaidi kutoa udhuru au kujitakasa katika dhambi mara nyingi ni wakali zaidi katika kuhukumu na kukemea wengine. Kuna wengi leo, kama Sauli, wakileta juu yao hasira ya Mungu. Wanakataa ushauri na kudharau maonyo. **Hata wakati ambao wanajua kuwa Bwana hayuko pamoja nao, wanakataa kuona ndani yao sababu ya matatizo yao**. Ni wangapi wanapenda roho ya kiburi na majivuno, anapohusika katika hukumu ya kikatili au kukemewa kwa ukali kwa wengine kuwa bora kwa wengine katika moyo na maisha kuliko wao. Vyema inaweza kuwa kwa mahakimu hawa wakujiweka kutafakari maneno hayo ya Kristo: "Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea."

Kujiinua, kujisifu kwa kile tumetenda au tunaweza fanya, ni ushahidi wa ujinga mkubwa au upumbavu. Wale ambao wanamakadirio yasiyofaa kujihusu mara nyingi wanaletwa katika nafasi ambayo tabia yao ya kweli itakuzwa. Ndivyo ilivyokuwa katika hali ya Sauli. Mwendo wake mwenyewe uliwafanya watu kuamini kwamba heshima na mamlaka ya kifalme zilikuwa muhimu kwake kuliko haki, rehema, au ukarimu.

Bwana huvumilia kwa muda mrefu upotovu wa wana wa Adamu, na huwapa wote fursa za kutosha za kuona na kuacha dhambi zao. Ila atadumisha utukufu wake mwenyewe, na utunzaji wa watu wake mwenyewe; hata mwendo wao wa uasi na kurudi nyuma ukiwa vipi. Anawezaonekana kufanikisha wale ambao wanapuuza mapenzi yake na kudharau maonyo yake; lakini kwa wakati wake mwenyewe hakika atadhihirisha upumbavu wao.

**Kwa uamuzi mmoja mbaya, watu wanaweza jiweka kwa hatari isiyosemeka. Kosa moja linaweza pelekea kwa maisha ya milele ya utunzaji, wasiwasi, na huzuni. Kama watu wa Israeli hawangeingilia kuokoa maisha ya Yonathani, shujaa huyu jasiri angeangamia kwa amri ya kiongozi waliyemchagua**. Ni kwa wasiwasi gani lazima watu hao wangemfuata mwongozo wa Sauli! **Ni ya uchungu aina gani mawazo kwamba alikuwa amewekwa kwenye enzi kwa matendo yao wenyewe!**

Watu wa Mungu wa leo wako katika hatari ya kutenda kosa lenye maafa. Hatuwezi, hatufai, kuweka imani ya kipofu kwa mtu yeyote, hata taaluma yake ya imani ikiwa ya juu kiasi gani au cheo chake kanisani. Hatupaswi kufuata uongozi wake, ila tu kama neno la Mungu linamdhibitisha. Mungu anataka watu wake binafsi watafautishe kati ya dhambi na haki, kati ya thamani na mbovu.

Wale ambao wanafanya kazi kwa uaminifu na kujitolea katika kazi ya Mungu wanapaswa kuheshimiwa sana kwa sababu ya kazi yao. Tunaweza, penda wana wa Israeli, kujaribu kubadilisha kazi yao ya kujitolea na kujikana nafsi kwa ile ambayo inaonekana kupendeza zaidi, lakini ambayo imani na udhabiti wake bado haujajaribiwa. Tutahadhari jinsi tunaonyesha kukosa shukurani au dharau kwa wale ambao Mungu ameweka kuwa wabeba mizigo katika kazi yake. Wale ambao hupiga askari wa msalaba wanapiga mkono wa Mungu ambao huwafunika kama ngao.

# 7. Watu Waliopotoka.

Baada ya kufikisha maonyo Gilgali, Samweli alikuwa na mabadilishano kidogo na mfalme wa Israeli. Sauli alichukia kukemewa kwa nabii, na akamuepuka kadri awezavyo; na Samweli hakuingilia uwepo wake au ushauri wake. Lakini Mungu alimwamuru kupeleka ujumbe mwingine kwa mfalme. **Mungu alikusudia tena kutenda kupitia kwa Sauli, kuwaangamiza adui wa Israeli**.[15]

Akitii agizo hili, nabii alimkumbusha kwamba alikuwa amepewa mamlaka na Bwana ya kumteua mfalme, na kwamba bado alinena kwa mamlaka sawa. Kisha alitangaza ujumbe takatifu. "Bwana wa majeshi asema hivi, **Nimeyatia moyoni mwangu[16] mambo hayo Amaleki waliyowatenda Israeli**, jinsi walivyowapinga njiani, hapo walipopanda kutoka Misri. Basi sasa enda ukawapige Amaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo, wala msiwaachilie."

Amaleki walikuwa watu wa kutangatanga ambao walikuwa wanaishi jangwani kusini mwa Palestina, katikati mwa nchi hiyo na Misri. Kama wengi wa makabila jirani, walikuwa waabudu sanamu, na adui wenye uchungu wa Israeli. Mara tu baada ya kutoka waliwavamia Waisraeli katika jangwa la Refidimu, lakini kiishara walishindwa na Yoshua. Amaleki hawakuwa miongoni

[15] Mungu alitenda kupitia kwa Sauli kwa namna ambayo alifikia maovu ya Waamaleki kwa uovu wa Sauli. Hakuna yeyote anayeweza kuthibitisha kuwa Sauli alikuwa na uhusiano sahihi na Mungu kwa hivyo Bwana analeta matukio mahali ambapo dhambi itaadhibu dhambi.

[16] Neno kumbuka hapa ni pâqad H6485. Ni neno sawa na kupatiliza katika Kutoka 20:5 nawapatiliza wana maovu ya baba zao. Hili linatoa ushahidi wa kupatilizwa kwa haki ya Mungu kwa kuadhibu dhambi kwa dhambi. Ataongoza matukio ya kuhakikisha kwamba watu wanavuna walichokipanda.

mwa mataifa ambayo inchi yao ilipeanwa kwa Israeli, wala walipokea majeraha yoyote kutoka kwao. Kwa hivyo, shambulio lilikuwa bila kuchochewa kabisa. Ilikuwa karibu uoga na ukatili; uadui, **bila kudhubutu uvamizi wazi na Waebrania, walikuwa wamevamia na kuua wale ambao walikuwa wameanguka kwa unyonge na uchovu nyuma ya miili ya wenyeji**.

Musa alikuwa ameamuriwa kudumisha rekodi ya vita, na pia adhabu ya mwisho ya ibada hiyo ya sanamu, kama ilivyotangazwa na Mungu mwenyewe: "nitaufuta ukumbusho wa Amaleki kabisa, usiwe tena chini ya mbingu, kwa sababu [kusoma kiasi] Mkono wa Amaleki ni dhidi ya enzi ya Yehova." Bwana wa dunia yote alikuwa ameweka enzi yake katika Israeli, na alikuwa ameonyesha nguvu na ukuu wa utukufu wake katika kuwatoa watu wake wateule katika utumwa wa Misri. **Amaleki walipowashambulia, walishambulia enzi ya Mungu, ambaye aliamua kuthibitisha mamlaka yake, kama onyo kwa mataifa yote ya baadaye.**

Baada ya kukataa hukumu dhidi ya Amaleki, Bwana alingoja kwa muda mrefu wageuke kutoka njia zao za uovu; lakini walizidi katika dhambi hadi uovu wao ulifikia urefu wake, hadi siku yao ya muda wa majaribio ikaisha, na **haki ya uungu ilidai uharibifu wao**.[17] Watu hao waovu walikuwa wakiishi katika ulimwengu wa Mungu, nyumba ambayo alikuwa ameandaa kwa wanawe waaminifu na watiifu. Ila waliweka karama yake kwa matumizi yao wenyewe, bila hata wazo moja la Mpaji. **Kadri alivyowamwagia mibaraka zaidi juu yao, ndivyo walizidi kuasi kwa uwazi zaidi dhidi yake**. Hivyo waliendelea kupotoa baraka zake na kutumia vibaya rehema zake. Walifanya mioyo yao imara katika uovu, lakini Mungu alikaa kimya; **na wakasema mioyoni mwao. "Mungu ajuaje?** Yako maarifa kwake aliye juu?" Lakini rekodi zao mbaya za uhalifu wao mara kwa mara zilikuwa zikipita hadi mbinguni. Kuna mpaka ambao wanadamu hawawezi endelea katika dhambi,--

"Mpaka uliofichika kati ya rehema ya Mungu na ghadhabu yake."

Wakati mpaka huo ulikuwa umevukwa, Mungu aliamka kwa ghadhabu yake kuwatoa kwa nyumba ambayo walikuwa wamechafua.

Mungu wetu mwingi wa neema bado huvumilia kwa muda mrefu wasiotubu. Huwapa nuru kutoka Mbinguni, ili waweze kufahamu utakatifu wa tabia yake, na haki ya mahitaji yake. Huwaita katika toba, na kuwahakikishia

---

[17] Zab 9:16 Bwana amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake.

hiari yake ya kuwasamehe. Lakini **kama wakiendelea kukataa rehema zake, mamlaka huenda mbele kuwatoa katika uharibifu**.[18]

Hivyo ndivyo ilikuwa na Sodoma. Tazama mji wakuogopewa wa tambarare, uliowekwa katika bustani ya uzuri. Kwa maono ya mwanadamu ni eneo la utulivu na usalama. Mashamba yenye rutuba yamejawa na mazao. Kuna wingi wa usambazaji wa kila kinachohitajika, karibu bila kazi yoyote. Milima iliyombali imefunikwa na makundi. Wafanyabiashara wa mashiriki wanaleta hazina zao kutoka mbali. Watu wanaishi kwa furaha na kufanya likizo moja ndefu ya mwaka.

Uvivu na utajiri ni laana yao. Wemefyonzwa katika shughuli za kilimwengu na furaha ya kidunia. Ila hakuna ishara inayoonekana ya ghadhabu ya Mungu inayoonekana ikiniginia juu ya mji uliojitoa. Siku yao ya mwisho ni kama zingine nyingi ambazo zimekuja na kuenda. Usiku wao wa mwisho hauonyeshwa na dhambi kuu zaidi kuliko zingine nyingi kabla yake. Lakini rehema, ambayo imekataliwa kwa muda mrefu, hatimaye hukomesha kuomba kwake. **Mioto ya kisasi cha uungu huashwa katika bonde la Siddimu**.[19] Mji wa Sodoma mzuri lakini wenye hatia unakuwa ukiwa, mahali ambapo kamwe hapawezi jengwa au kukaliwa.

Moto ambao uliila miji ya tambare ulimwaga nuru ya maonyo yake hata kwa wakati wetu. Unatuagiza tuachane na dhambi ambazo zilileta uharibifu juu ya waovu siku hiyo.

Mungu anahitaji huduma ya viumbe vyake vyote. Kila kitu katika maumbile hutii mapenzi yake. Mbingu zisizo na viwango huwaka kwa utukufu wake. Vyote katika vile ambavyo ameumba juu ya dunia, mwanadamu tu huasi dhidi ya Muumbaji. Watu wadhaifu, wapotovu, viumbe vya saa moja, wanadhubutu

---

[18] Mungu hudumisha hesabu pamoja na mataifa. Sio hata shomoro huanguka pasipo kutambua. **Wale ambao hupanga maovu kwa wenzao, wakisema, Mungu atajuaje? Siku moja wataitwa wakutane na kisasi kilichohairishwa kwa muda mrefu**. Katika kipindi hiki zaidi ya dharau la kawaida linaonyeshwa kwa Mungu. Wanadamu wamefikia mahali katika dhuluma na uasi ambapo panaonyesha kuwa kikombe chao cha uovu kiko karibu kujaa. Wengi karibu wanavuka mipaka ya rehema. Hivi karibuni Mungu ataonyesha kuwa kweli ndiye Mungu aishiye. Atawaambia malaika, "**Msiendelee tena kupambana na Shetani katika jitihada zake za kuangamiza. Wacha atekeleze ukorofi wake juu ya wana wa uasi; kwa kuwa kikombe cha uovu wao kimefurika**. Wamefuzu kutoka shahada moja ya uovu hadi nyingine, wakiongeza kila siku kwa uvunjaji wa sheria wao. Kamwe sitaendelea kuingilia kati kumzuia mharibifu kutekeleza kazi yake." {RH, Septemba 17, 1901 par. 8}

[19] Ibid

kuingia katika mgogoro na wa Kudumu, Chanzo cha hekima yote na nguvu zote. Wale ambao daima wanategemea fadhila za Mungu, wanadhubutu kudharau Mkono ambao mibaraka yao hutiririka kwao. Hakuna ukosefu wa shukurani muovu zaidi, hakuna upofu kamilifu zaidi, kama ule wa watu ambao hukataa kuthamini wajibu wao kwa Mungu.

Watu sio wakaazi tu wa nyumba kuu ya Mungu, na washirika wa neema yake, bali ni vitu vya utunzaji na upendo wake usiokoma. Huifanya kuwa fadhila yao, kupitia kwa haki ya Kristo, kumuita Baba. Wanaweza omba mibaraka yake kuu bila kumaliza hazina za neema yake. Katika kutojua kwao wanaweza ongozwa kwa mashauri ya hekima sahihi. Katika msiba wanaweza jikinga chini ya kivuli cha enzi yake, na kuwa salama katika pahali pa siri.

Mungu huyu mwenye nguvu anaahidi neno lake lisilobadilika kwamba wale wanaompenda na kumuamini hawatapungukiwa na kitu chochote kizuri. **Lakini anatangaza kwamba hakika ataadhibu waasi wa sheria yake. Uovu wa jamaa hausahauliki au kupuuziliwa kwa sababu Mungu hawapatilizi mara moja kwa hukumu**.[20] Kila karne ya uasherati na uasi inaweka hazina ya ghadhabu dhidi ya siku ya ghadhabu.

Wakati Waandishi na Mafarisayo walikataa mafundisho ya Kristo, aliwaambia wamejaza uovu wa baba zao, ili iwe wakati wa Mungu kutenda kazi; kwamba ujumbe habari za furaha ziweze kufikishwa kwa wengine, ambao wataipokea kwa furaha. Wakati hatimaye uvumilivu wa uungu uliisha, ghadhabu ya Mungu ilianguka kiishara juu ya wale ambao walikuwa wameikataa nuru yake kuu.

**Mungu hafurahi ulipishaji wa kisasi, ingawa hutoa hukumu kwa waasi wa sheria yake. Analazimishwa kufanya hili, ili kukinga wenyeji wa dunia kutoka kwa kuharibiwa na kuangamizwa kabisa. Ili kuokoa baadhi, lazima, awakatilie mbali wale ambao wamefanywa wagumu katika dhambi**.[21] Asema nabii Isaya: "Maana Bwana ataondoka kama vile katika mlima Perasimu,

---

**20** Nilionyeshwa kwamba hukumu ya Mungu haitatoka kwa Bwana moja kwa moja juu yao, bali kwa njia hii: Wanajiweka ambapo hawezi walinda. Anaonya, anarekebisha, anakaripia, na anaonyesha njia pekee ya usalama; kisha wale ambao wamekuwa wahusika wa huduma yake ya pekee watafuata mwendo wao wenyewe huru kutoka kwa Roho wa Mungu, baada ya maonyo, wakichagua njia yao wenyewe, basi hawaagizi malaika wake kuzuia uvamizi ulioamuliwa na Shetani juu yao. 14MR 3

21 Swali ni je, Mungu anawakatilia vipi? Sentensi inayofuata katika aya hii inadhihirisha mchakato huo.

ataghadhibika kama vile katika bonde la Gibeoni; apate kufanya kazi yake, kazi yake ya ajabu; na kulitimiza tendo lake, tendo lake la ajabu.” **Kazi ya ghadhabu na uharibifu kwa kweli ni kazi ya ajabu, kazi isiyokaribishwa kwake yeye aliye na upendo usio na mwisho**.[22]

Tena, ujumbe mtakatifu unamjia Ezekieli: “Kama Mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, sikufurahii kufa kwake mtu mwovu; bali aghairi mtu mwovu, na kuiacha njia yake mbaya, akaishi.” Uhalisia hasa kwamba Mungu hapendi kuwaadhibu wenye dhambi unaonyesha ubaya wa dhambi ambao huhitaji hukumu yake. Na ila kwa kila muasi wa sheria yake takatifu kunatolewa wito huu wa kusihi, “Ghairini, ghairini, mkaache njia zenu mbaya; mbona mnataka kufa?”

Rekodi za historia takatifu zinatangaza, ingawa Mungu ni Mungu wa haki, mkali kwa kuona uovu, na mwenye nguvu za kuadhibu mdhambi, pia ni Mungu wa kweli, mwenye huruma, na mwingi wa rehema. **Wakati anapatiliza hukumu[23] dhidi ya waasi wa sheria yake na adui wa watu wake, atawalinda wale ambao wanaheshimu maagizo yake na kuonyesha ukarimu kwa wateule wake**.

**Wakati aliamuru kwamba vita ya kuangamiza kabisa ipiganwe dhidi ya Amaleki[24]**, pia aliamuru kwamba Wakeni, ambao wanakaa ndani yao, wahifadhiwe, kwa sababu walikuwa wamewahurumia Israeli katika dhiki yao. Yethro, mkwewe Musa, na mfalme miongoni mwa Wakeni, alikuwa amejiunga na Israeli muda mfupi baada yao kutoka Misri. Uwepo wake na ushauri wakati huo ulikuwa wa thamani kubwa kwa Waebrania. Musa baadaye alimsihi Hobabu, mwana wa Yethro, kuongozana nao katika safari yao kupitia jangwani, akisema: “Sisi twasafiri kwenenda mahali ambapo Bwana amenena habari zake hivi, Nitawapa ninyi mahali hapo; uje pamoja nasi, nasi tutakufanyia mema; kwa kuwa Bwana ametamka mema juu ya Israeli.”

---

[22] Tazama kijitabu. Tendo la Mungu la Ajabu. Neno la kwanza *ajabu* linamaana ya kuenda kinyume. Mara ya pili neno linamaanisha kuwa mgeni wa usiyemjua. Tendo la Mungu la Ajabu ni kuruhusu wanawe waliopotea kupokea athari za uchaguzi wao. Hili linauma kwa Mungu kufanya hivi. Ila, atalifanya kwa haki madhubuti.

[23] Zingatia matumizi ya neno *patiliza*. Mungu anapatiliza hukumu hii kulingana na Kut 20:5 inayopatikana katika amri ya pili. Anawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wale wanaomchukia. Hii inamaana anasimamia mchakato wa dhambi ikiadhibu dhambi.

[24] Agizo hili ni onyesho la mawazo binafsi ya Sauli kupitia mchakato ambao tutaona karibuni.

Hobabu alikataa, akichagua kuishi katika nchi yake mwenyewe na miongoni mwa watu wake mwenyewe. Lakini Musa alijua kwamba mkwewe alifahamiana vizuri na nchi ambayo wangepitia, na kwamba angewasaidia sana katika safari yao. Kwa hivyo alimuomba kwa bidii: "Usituache, tafadhali; kwa kuwa wewe wajua jinsi tutakavyopanga nyikani, nawe utakuwa kwetu badala ya macho. Itakuwa, ukienda pamoja nasi, naam, itakuwa mema yo yote Bwana atakayotutendea sisi, tutakutendea wewe vivyo." Hobabu alikubaliana na hili; lakini kusafiri kwa Israeli kwote, yeye na wafuasi wake waliwaacha majirani wa miji, na wakajirasimu kwa hewa huru, katika jangwa la Yuda, katika mpaka wa kusini wa Kanani.

Ahadi ya ulinzi wa kipekee na urafiki iliyotolewa na Musa kwa Wakeni, ilitolewa kwa maagizo ya Bwana. **Hivyo Sauli alipoagizwa kuangamiza Waamaleki, maagizo ya kipekee yalitolewa kwamba Wakeni wasiangamizwe. Yethro na familia yake walikuwa waabudu wa kujitolea wa Mungu wa kweli;**[25] lakini ingawa Waakeni walikua marafiki wa Israeli, na walithamini Mungu aishiye kama mtawala wa dunia, dini yao ilikuwa imechafuliwa na ibada ya sanamu. Baada ya wakati huu walikuwa wameingia zaidi kabisa katika upagani, na athari yao ikawa mtego kwa Waebrania. Hivyo hatimaye walipatilizwa na hukumu takatifu.

Balaamu, kwa muongozo wa Roho Mtakatifu, alitabiri kuharibiwa kwa Wakeni na Waamaleki: "Kisha akamwangalia Amaleki, akatunga mithali yake, akasema, Amaleki alikuwa ni wa kwanza wa mataifa; Lakini mwisho wake atafikilia uharibifu. Kisha akamwangalia Mkeni, akatunga mithali yake, akasema, Makao yako yana nguvu, Na kitundu chako kimewekwa katika jabali. Pamoja na haya Wakeni wataangamizwa, Hata Ashuru atakapokuchukua mateka. Akatunga mithali yake akasema, Ole wao! Ni nani atakayepona, Mungu atakapofanya haya?"

## 8. Jaribio la Mwisho.

Kuwashinda Wafilisti kule Mikmashi kulionekana kama hatua ya kugeuka katika bahati ya Israeli. **Ingawa Bwana alikuwa amekasirika na Sauli, na akakusudia kuitenga familia yake, ila alimpa mafanikio katika vita dhidi ya watesi wa watu wake**. Hakuna adui aliyeonekana kuweza kusimama dhidi

[25] Bila shauri hili la kipekee, Sauli angewaangamiza pia.

yake. Alifanya vita wakati huo dhidi ya Moabi, Ammoni, na Edomi, **na dhidi ya Waamaleki**[26] na wafilisti; na alipogeuza mkono wake, alipata ushindi. Ila, akiwa ameikosa fursa ambayo Mungu alikuwa amempa, kamwe hakuweza kuwashinda wafilisti kwa ushindi wa kudumu. Alikuwa na vita vya kuumiza nao siku zote za maisha yake.

**Alipoamriwa kuwaangamiza Waamaleki, Sauli hakusita hata kidogo. Kwa mamlaka yake mwenyewe aliongezewa amri ya nabii, na kwa wito wa kupigana waume wa Israeli walikusanyika kwa kiwangogezi chake**.[27] Watu elfu mia mbili waendao kwa miguu, na kisha watu elfu kumi wa Yudah walihesabiwa Telaim. Kwa nguvu, Sauli alivamia na kumshinda mfalme wa Waamaleki, na wakatawala nchi.

Ushindi huu ulikuwa kwa mbali zaidi mkuu ambao Sauli aliweza kupata daima, na ulifanya kuwasha upya hicho kiburi cha moyo ambacho kilikuwa hatari yake kuu. Amri takatifu ikitoa Amaleki kwa uharibifu kabisa ilitekelezwa kwa kiwango tu. Tamaa ya kukuza heshima ya marejeo yake ya ushindi kwa uwepo wa mfalme aliyetekwa nyara, Sauli alitafuta kumhifadhi Agagi, mfalme katili na mpenda vita wa Amaleki.

**Tendo hili halikuwa bila athari kwa watu. Wao pia walihisi kwamba pia wanaweza jiingiza katika kuondoka kiasi kutoka kwa maelekezo wazi ya Bwana na wawe salama. Kwa hivyo kwa tamaa walibakisha kwao makundi, ng'ombe, na wanyama wa mizigo, na kuangamiza wale tu waliokuwa wabovu na wadhaifu.** [28]

Hapa Sauli alikuwa amewekwa kwa jaribio la mwisho. Kupuuza kwake kwa kiburi mapenzi ya Mungu, akionyesha uamuzi wake wa kutawala kama mfalme huru, kulidhihirisha kwamba hawezi kabidhiwa nguvu za kifalme mwakilishi wa Bwana. Bila kujali yote haya, Sauli anakuza jeshi lake la ushindi, na pamoja na mfalme aliyetekwa nyara na kundi kubwa na ng'ombe wengi--ngawira

---

[26] Zingatia kwa makini kwamba Sauli tayari alikuwa vitani na Amaleki kabla ya agizo kuja 1 Sam 15:1-3

[27] Agizo la Mungu liliongezea kwa mamlaka ya Sauli mwenyewe. Sauli tayari alikuwa vitani na Amaleki lakini Mungu analeta kichocheo cha Sauli kuendeleza kile ambacho tayari alikuwa akifanya katika sura ya mawazo ya aliye katika uasi dhidi ya Mungu.

[28] Tendo la Sauli la kumuacha Agagi linatupa mfano kwa watu wake kuhifadhi mateka wa vita kinyume na kile walifahamu kilikuwa agizo la Mungu.

iliyoheshimiwa sana mashariki--iliwekwa mbele kwenye msafara kuelekea nyumbani. Kule kameli, kwa umiliki wa Yuda, alijenga mnara kwa ushindi wake.

Kiburi na kufurahia zilipokuwa zikitawala katika kambi ya Sauli, kulikuwa na uchungu mwingi nyumbani mwa Samweli. **Hamu yake kuu ya ustawi wa Israeli haikuwa imekoma. Bado alipenda shujaa shupavu ambaye mikono yake mwenyewe ilikuwa imemteua kama mfalme. Lilikuwa ombi lake la moyoni kwamba Sauli aweze kuwa kiongozi mwenye hekima na kunawili. Alipodhihirishiwa kwamba hatimaye Sauli alikuwa amekataliwa, Samweli katika dhiki yake "akamlilia Bwana usiku wote," akisihi hukumu ibadilishwe**.[29] Kwa moyo wenye kuuma alianza safari asubuhi iliyofuatia kukutana na mfalme aliyekosea. Lakini aliposikia kwamba Sauli alikuwa ameweka mnara wa ushujaa wake mwenyewe, badala ya kumtukuza Mungu, aligeuka na akaenda Gilgali.

Huko mfalme na jeshi lake alikuja kukutana naye. Samweli alitamani kwa tumainio kubwa kwamba Sauli angeweza, kwa kutafakari, kufahamu dhambi yake, na kwa kutubu na unyenyekevu kwa Mungu, arejeshwe tena kwa fadhila takatifu. Lakini mfalme alisonga mbele kwa hakikisho kuu, akisema, **"Ubarikiwe na Bwana, nimeitimiza amri ya Bwana." Sauli alikuwa ametekeleza matakwa yake mara nyingi, bila kuzingatia amri ya Mungu kupitia kwa nabii, kiasi kwamba mtazamo wake wa kimaadili ulikuwa umetiwa giza. Sasa hakuwa na ufahamu wa uovu wa mwenendo wake.** [30]

Sauti ambazo zilianguka masikioni mwa nabii, zinapinga kauli ya mfalme asiyetii. Kwa swali lililoulizwa, "Maana yake nini, basi, hiki kilio cha kondoo masikioni mwangu, na huu mlio wa ng'ombe ninaousikia?" Sauli akasema, "Wamewaleta kutoka kwa Waamaleki; maana watu waliwaacha hai kondoo na ng'ombe walio wazuri, ili wawatoe dhabihu kwa Bwana, Mungu wako, nao waliosalia tumewaangamiza kabisa." Ombi lililoombwa hapa lilikuwa zuri lakini udhuru wa kutamani. Wanyama waliookolewa kwa uharibifu wangetolewa na Waisraeli badala ya wanyama wao wenyewe waliohitajika kwa sadaka.

Roho ambaye aliyemwendesha Sauli anaamushwa na ukweli kwamba wakati anajigamba kwa kiburi kwa utiifu wake kwa amri takatifu, anajichukulia

---

[29] Kwa ajabu tu. Upendo wa Samweli kwa sauli na kuombea maisha yake kulidhihirisha tabia ya Kristo.

[30] Mtazamo wa kishaba wa Sauli, uongo ambao alitamka na mtazamo wa wanyama wote kungemsababishia Samweli huzuni kubwa. Hasa vile alikuwa macho usiku wote akimlilia Sauli na kuomba abadilike. Kisha kuona kilele cha uasi ingekuwa ngumu zaidi kwa Samweli.

heshima yote; anapokaripiwa kwa kutotii, anaweka dhambi kwa watu. Samweli hakudanganyika kwa udhuru wa mfalme. Kwa mchanganyiko wa huzuni na ghadhabu anatangaza, “Ngoja, nami nitakuambia neno aliloniambia Bwana usiku huu.” Kisha akamkumbusha Sauli kuhusu unyenyekevu wake wa awali: “Ingawa ulikuwa mdogo machoni pako mwenyewe, je! Hukufanywa kuwa kichwa cha kabila za Israeli?” Anarudia amri takatifu kuhusiana na Waamaleki, na anadai kutoka kwa mfalme sababu ya kutotii kwake.

Sauli kwa ukaidi wake anasisitiza katika kujitakasa; “Hakika mimi nimeitii sauti ya Bwana, nami nimemleta Agagi, mfalme wa Waamaleki, tena nimewaangamiza Waamaleki kabisa. Ila watu waliteka nyara, kondoo na ng'ombe walio wazuri, katika vitu vilivyowekwa wakfu, kusudi wavitoe dhabihu kwa Bwana, Mungu wako, huko Gilgali.” Kama Sauli mwenyewe angetii amri za Mungu, na kuitekeleza miongoni mwa watu kwa uwamuzi sawa na ule ambao alikuwa amedhihirisha katika kutenda amri zake, hangekuwa na ugumu wowote kupata utiifu. Mungu alimchukulia kuwa kisababishi cha dhambi ambazo kimsingi alijaribu kuhukumu juu ya Israeli.

Kwa maneno makali na ya makini nabii wa Aliye Juu anafagia kambi ya uongo, na anatangaza dhidi ya sauli kauli isiyoweza tenguliwa: “je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu Sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu, mfalme **Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi,**[31] Na **ukaidi ni kama ukafiri na vinyago**; Kwa kuwa umelikataa neno la Bwana, Yeye naye amekukataa wewe usiwe mfalme.”

Mfalme aliposikia kauli hii ya kutisha, akalia, “Nimefanya dhambi; maana nimeihalifu amri ya Bwana, pia na maneno yako; kwa sababu naliwaogopa wale watu, nikaitii sauti yao.” Sauli alijawa na hofu ya kukataliwa na nabii, lakini alikuwa, hata sasa, hisia za kweli za ubaya wa uasi wake. Bado alisisitiza kuwawekea watu lawama, akitangaza kwamba alikuwa ametenda dhambi kwa kuwaogopa.

Huu ulikuwa udhuru sawa uliotolewa na Haruni kujizuia kutoka kwa kosa la kutengeneza ndama wa dhahabu. Lakini hadi wakati huo kutokana na kukubali

[31] “Samweli alimwalifu Sauli kwamba uasi wake ulikuwa dhambi ya uchawi. Kwamba, wakati mtu alianza kufuata njia ya uasi, anajiweka wazi kwa athari ya kile ambacho ni pinzani na mapenzi ya Mungu. Shetani hutawala mawazo ya uasi.” 4aSG 76

udhuru, **Musa kwa ukali alimkemea Haruni, mbele ya watu wote**.[32] Kama kuhani mkuu wa Israeli, na mwakilishi wa Musa wakati hayupo, Haruni kwa hatari yoyote ile angepinga mtindo wa haraka na kinyume cha Mungu wa watu. Mapuuza yake ya kufanya hivi yalileta dhambi juu yao, majanga, na maangamizi, ambayo hakuwa na uwezo wa kugeuza. Ilikuwa rahisi kuwaongoza katika kutenda dhambi, lakini alitafuta kwa bidii bila mafanikio kuwaongoza katika kutubu. Musa baadaye alitangaza, "Bwana alimkasirikia sana Haruni akataka kumwangamiza." Dhambi yake ingeadhibiwa kwa kifo kama hangejinyenyekeza kwa toba ya kweli mbele za Bwana. Kama Sauli, kwa namna sawa, angekuwa tayari kuona na kutubu dhambi yake, yeye pia angesamehewa.

Haikuwa huzuni kwa sababu ya dhambi, bali hofu ya ghadhabu yake ndio ilimsukuma mfalme wa Israeli alipomwomba Samweli, "Nakuomba, unisamehe dhambi yangu; rudi pamoja nami, nipate kumwabudu Bwana."

"Sitarudi pamoja nawe," lilikuwa jibu la nabii; "Kwa sababu umelikataa neno la Bwana, Bwana naye amekukataa wewe, usiwe mfalme wa Israeli." **Samweli alipogeuka kuondoka,[33] mfalme katika masumbuko ya hofu, alishikilia joho yake ili kumrejesha, lakini iliteleza mkononi mwake. Juu ya hili, nabii alitangaza, "Leo Bwana amekurarulia ufalme wa Israeli, naye amempa jirani yako, aliye mwema kuliko wewe**." Akijua jinsi maneno yake yalikuwa yamechukuliwa kwa urahisi na mfalme, anaongezea hakikisho dhabiti, "Tena Yeye aliye Nguvu za Israeli hatanena uongo, wala hataona majuto." Sauli alikuwa amejitukuza katika ushujaa wake, kana kwamba alikuwa mwokozi wa watu wake. Nabii anakemea kiburi hiki kwa kumkumbusha mfalme mwenye kiburi kwamba Mungu alikuwa nguvu ya Israeli.

Hata sasa Sauli anaogopa tu aibu binafsi na kupoteza ufalme wake. Anasumbuliwa zaidi na ukengeufu wa Samweli kuliko na kukasirika kwa Mungu. Alimsihi Samweli amsamehe uovu wake, kana kwamba nabii alikuwa na uwezo wa kubadili hukumu takatifu dhidi yake. **Alijua kwamba watu walikuwa na imani dhabiti kwa Samweli kumliko. Kama mfalme mwingine**

[32] "Musa alipoona Ibada ya sanamu ya Israeli na hasira yake ikaamshwa na jinsi walimsahau kwa haya Mungu kwamba alitupa chini mawe na kuzivunja, Haruni alisimama kando yake kwa upole, akibeba lawama ya Musa kwa uvumilivu wa kupondezwa. Watu walipendezwa na roho wa kupendeza wa Haruni na walikasirishwa na kasi ya Musa. Lakini Mungu haoni kama mwanadamu aonavyo. Hakukemea shauku wala hasira ya Musa dhidi ya uasi uliokithiri wa Israeli." {3T 300.3}

[33] Samweli alitaka kuondoka. Wakati huu hakuwa amepanga kumuua Agagi.

**angeteuliwa kwa amri takatifu, alihisi kwamba hatima yake mwenyewe haikuwa na tumaini. Kama Samweli angemkataa na kumuacha, aliogopa uasi wa mara moja miongoni mwa watu.**

**Kama uasi wa mwisho, Sauli alimuomba nabii kumpa heshima mbele ya wazee na watu kwa kuunganika naye hadharani katika kumwabudu Mungu. Samweli alisalia,**[34] **tu kama mtazamaji tuli wa huduma hii**. Bila unyenyekevu au toba, ibada ya Sauli haingekubalika kwa Bwana.

**Tendo la dhuluma, kali na kutisha, bado lilikuwa litendeke. Samweli lazima athibitishe hadharani heshima ya Mungu, na kukemea mwenendo wa Sauli**.[35] Anaamrisha kwamba mfalme wa Amaleki aletwe mbele yake. Zaidi kwa wale wote ambao walikuwa wameanguka kwa upanga wa Israeli, Agagi alikuwa mhusika kama mtetezi wa msingi wa upagani wa watu wake, na mwanzilishi wa uasi wao wa kikatili; ilikuwa tu kwa hilo lazima angeangukiwa na ghadhabu nzito. Alikuja kwa amri ya nabii, katika kiburi cha kifalme, akijigamba kwamba angeweza kusimamisha mtumishi wa Mungu, na kwamba hatari yote ya kifo ilikuwa imepita. **Maneno ya Samweli yalifukuza hakikisho lake: "Kama upanga wako ulivyofanya wanawake kufiwa na watoto wao, vivyo hivyo mama yako atafiwa miongoni mwa wanawake Basi Samweli akamkata Agagi vipande mbele za Bwana**."[36] Hili likiwa limetekelezwa, Samweli alirudi nyumbani kwake Rama, na Sauli kwake Gilgali. Nabii na mfalme hawakuwa wakutane tena.

Samweli alikuwa mtu mwenye wingi wa huruma ya moyo, na upendo mkubwa, kama inavyodhibitishwa na huzuni ambayo alihisi alipoagizwa kutangaza hukumu takatifu dhidi ya Sauli. Ila alipohitajika kutekeleza haki dhidi ya mfalme muovu wa Amaleki, alitekeleza kazi isiyoyakukaribishwa bila

---

[34] "Kwa mwelekezo takatifu Samweli alisikiliza ombi la mfalme." PP 632

[35] Tendo la Sauli la kumhifadhi agagi liliwafanya watu kuamini kuwa wanaweza kosa kutii maelekezo ya Mungu wapendavyo. Kama tulivyosoma awali "Tendo hili halikuwa bila athari kwa watu. Wao pia walihisi kwamba wao pia wanaweza jiingiza katika kuondoka kiasi kutoka kwa maelekezo wazi ya Bwana na wawe salama."

[36] Mkazo ambao samweli alimkata agagi vipande unanena kuhusu jitihada ambayo kwayo alichukua kitendo hiki. Tunakumbuka maneno ya Bwana kwamba *atakumbuka au atapatiliza* matendo ya Amaleki. Hukumu hizi zote ziko chini katika muktadha wa kupatiliza uovu kwa uovu. Hakujatajwa amri ya moja kwa moja kutoka mbinguni ya kutekeleza kitendo hichi. Ingawa ili watu waje kwa ufahamu sahihi, Mungu alifanya kupitia kwa matukio kuona kwamba haki ilifahamika kutendwa.

kulegea. Lazima angedumisha uaminifu wake kwa Mungu, hata kukana hisia binafsi kukiwa kukuu namna gani.

Kuna tofauti pana jinsi gani kati ya matendo ya Samweli na mkondo ambao mfalme wa Israeli alifuata. Ili kutekeleza kusudi lake, Sauli angekua katili zaidi; **lakini wakati amepewa agizo takatifu la kuangamiza kabisa waasi, anapiga waliokuwa wahalifu wadogo, na kuacha yule ambaye laana ya Mungu ilikuwa juu yake hasa. Katika kiburi chake cha moyo alijigamba kwamba alikuwa na huruma zaidi kuliko Muumbaji wake**. Kwa mkondo huu wa tendo alitangaza hitaji takatifu kuwa dhalimu na katili.

Hali ya Sauli inapaswa kuwa funzo kwetu, kwamba maneno ya Mungu yanapaswa kuheshimiwa na kutiiwa. Uhalifu wote na majanga yote ya Israeli ya kale yalitokea kwa mapuuza yao ya kusikiliza maagizo ya Mtawala wao mtakatifu. Hapa kuna hatari yetu. Lazima tusikilize kwa bidii kile ambacho Bwana amenena, hata katika ikionekana kwa masuala madogo. Mungu anahitaji watu wake sio tu kusikia maneno yake, bali kutii kwa moyo wote. Kuzingatia maagizo ya Bwana wakati yanaingiana na mahitaji yetu wenyewe, na kuyapuuza wakati hili linafaa kusudi letu vizuri, ni kufuata mkondo wa Sauli. Kiburi katika mafanikio yetu wenyewe au kuzingatia kwa ukaidi matakwa yetu wenyewe, hufanya taaluma iliyotukuka zaidi au huduma ya kifalme kuwa machukizo machoni pa Mungu.

## 9. Kutii Ni Bora Kuliko Dhabihu.

"Kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu. Kwani kuasi ni kama dhambi ya uchawi, Na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago." Maneno haya ya ushauri, yakinenenwa na nabii Samweli kwa mfalme Sauli, yanafunzo ambalo linapaswa kufikiriwa na watu wa Mungu katika kila kizazi. **Sadaka ya kutoa dhabihu ya wakati wa zamani haikuwa na maana machoni pa Mungu. Wale ambao waliwasilisha dhabihu mbele za Bwana lazima wangekuwa na maana halisi ya agizo lake, wakikubali hali yao potovu kama wenye dhambi, na kukubali kifo cha Kristo kwa niaba yao. Lazima watubu uasi wao wa sheria ya Mungu, na kuonyesha imani katika Yesu kama ambaye tu anayeweza kuwaondolea.[37] Wakati sadaka ya dhabihu ilibadilishwa na kweli, hiyari, huduma ya furaha kwa Mungu, wakati ambao ilichukuliwa**

[37] Sawia na vile tufanyavyo leo.

**kuwa na umuhimu na sifa ndani yake, au wakati aina iliinuliwa zaidi ya kitu mfanowe, basi ilifanywa chukizo kwa Bwana.**

Kama Sauli angetoa dhabihu ya gharama kubwa, kutoka kwa kundi lake, akitubu kwa kila namna kilichohitajika katika sheria, ila katika roho ya kujitosheleza, na bila uvumilivu wa kweli, dhabihu yake ingekataliwa. Lakini wakati ambao alitoa mateka ya Amaleki, ambayo laana ya kiungu ilikuwa umetangazwa juu yake, ni jinsi gani tendo lake lilikuwa chukizo zaidi machoni mwa Mungu mtakatifu. Alikuwa amedhani, mbele ya Israeli, kuonyesha dharau kwa mamlaka ya Muumbaji wake.

"Kutii ni bora kuliko dhabihu." Funzo hili lina umuhimu wa kipekee kwa wakati wa sasa, wakati ambao madai ya sheria ya Mungu yanahimizwa juu ya uangalifu wetu. **Nuru sasa iking'aa kutoka kwa maneno takatifu inadhihirisha ukweli kwamba nguvu ya kigeni imeharibu amri za Yehova. Papa, "mtu wa dhambi," amejaribu kubadili majira na sheria zilizoamuliwa kwa nguvu za kiungu**. Muumbaji wa mbingu na nchi aliamuru, "Siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote." **Amri hii ilitekelezwa kwa mfano wa Mwanzilishi wake**, alitangaza kwa sauti yake mwenyewe, na akaweka katika kifua hasa cha amri. Lakini utawala wa papa umeondoa amri hii takatifu, na kubadilisha siku ambayo Mungu hajatakasa, na ambayo hakuipumzika, sherehe ambayo iliheshimiwa kitambo na watu wa mataifa kama "siku ya jua yenye heshima."

Katika haya yote, Shetani ndiye roho mkuu. Hana uhusiana hasa na Jumapili, lakini anataka kwamba mapenzi yake yaheshimiwe, badala ya mapenzi ya Mungu. Ni Shetani ndiye alimchochea Adamu na Hawa kuasi agizo la Muumbaji wao, na anaendeleza kazi hii hata kwa siku zetu. Tunaona kufanikiwa kwa shambulizi lake juu ya sheria ya Mungu, katika kutotambua kuliko enea kote kwa Sabbato ya kale ya Yehova, na kuheshimu kote kwa taasisi ya kipagani na kipapa. Na tunaona matokeo ya kutisha, katika wasiwasi kuhusu ukweli ambao unatawala kote. Sabbato ilianzishwa Edeni, kama kumbukumbu ya uumbaji. Inawaelekeza wanadamu moja kwa moja kwa Mungu wa kweli kama Muumbaji wa mbingu na dunia. Kwa hivyo inasimama kama nguzo yenye nguvu dhidi ya sanamu, ukanaji Mungu, na ukafiri. Kama Sabbato ingetunzwa kote, hakuna hata moja ya uovu huu ungepata nafasi katika ulimwengu wetu. Hakungekuwa na kafiri wala mwabudu sanamu.

Hata kanuni za kisiasa alizopewa Musa alipokuwa katika mkutano wa siri na Yehova, zinamafundisho muhimu kwa watu wa vizazi vyote. Lakini sheria iliyotangazwa kutoka Sinai umati wa watu wa Israeli ukisikia, na kuandikwa

kwa chanda cha Mungu, ni lazima juu ya watu wote tukikaribia mwisho wa wakati.

Wakati Mungu alimwagiza Sauli kuangamiza kabisa Amaleki, hakuachia Sauli uamuzi wa kuangamiza au kuacha hai kama atakavyoona vyema. Alipowakataza wazazi wetu wa kwanza kula kutoka kwa mti wa ujuzi wa mema na mabaya, hakuwaachia kula au kutokula, kama ilivyowapendeza. Alipowaamuru watu kuitakasa siku ya saba, hakuifanya hiari kwao kutubu kama ni sawa, na kama sio watakase siku ya uchaguzi wao.

Wengi hujitahidi kukwepa madai ya amri ya nne kwa kusihi kwamba sheria ya Mungu ilitolewa kwa Wayahudi peke; kwamba siku ya saba ya juma ni ya Wayahudi, wakati ambao siku ya kwanza ni Sabbato ya Wakristo. Tofauti hii haitambuliwi na Maandiko. **Hakuna tofauti kama hiyo kama inavyodaiwa kuwepo kati ya agano la Kale na Jipya, Sheria ya Mungu na injili ya Kristo, toleo la mahitaji ya Wayahudi na yale ya Wakristo**. **Kila roho iliyookolewa katika toleo la awali iliokolewa na Kristo kama hakika tunavyookolewa naye leo. Wazee na manabii walikuwa Wakristo.** Ahadi ya injili ilitolewa kwa joho ya kwanza Edeni, wakati walikuwa kwa uasi wamejitenga kutoka kwa Mungu. **Injili ilihubiriwa kwa Ibrahimu. Waebrania wote walikunywa kutoka kwa mwamba ule wa kiroho, ambao ulikuwa Kristo**. Ilikuwa katika Kristo ulimwengu wote uliumbwa. **Kwa Kristo Sheria ilitangazwa kutoka Sinai. Kwa hivyo, Kristo ni, katika maana kamili, kama anavyojitangaza kuwa, “Bwana wa Sabato.” Aliifanya siku kuwa takatifu kwake, ambayo kwayo atapokea ibada kutoka kwa malaika na wanadamu.**

Anawezaje dhubutu yeyote, akielewa madai ya amri ya nne, kukanyaga mahitaji yake? Sauli alisema, kama udhuru kwa uovu wake, kwamba “naliwaogopa wale watu.” Kuna wengi katika siku zetu, hata miongoni mwa wale wanaojiita mawaziri wa Kristo, ambao wanaweza to sababu isiyo bora kwa mkondo wao? Ingawa neno la Mungu liko wazi, hawadhubutu kukosea chuki yao au kusisimua hofu ya wasikilizaji wao; kwa hivyo wanawaacha bila kuonywa kwa uasi wao wa sheria ya Mungu. Katika siku ya hukumu ya mwisho udhuru wa Sauli utatolewa kwao sio tofauti kuliko ulivyotolewa kwake.

“Kuasi ni kama dhambi ya uchawi, Na ukaidi ni kama ukafiri na vinyago.” Uasi ulianza na Shetani. Bila kujali cheo cha juu alichokuwa nacho mbinguni, alikosa kuridhika kwa sababu hakupewa heshima kubwa. Hivyo akaswali kusudi la Mungu na akalalamikia haki yake. Alielekeza nguvu zake katika kuvutia malaika kutoka kwa utii wao. Ukweli kwamba alikuwa malaika mkuu, mwenye utukufu na nguvu, ulimwezesha kuweka athari kuu. Malalamishi yake

dhidi ya utawala wa Mungu, mara ya kwanza hayakupendelewa, ila kwa kurudiwa tena na tena, hatimaye yalikubalika na wale awali walikuwa waaminifu na kufurahia utawala wa Mfalme wa Mbinguni. Hakukuwa na kivuli cha uhalali au udhuru wa kutopendezwa; lakini chuki na wivu, mara ilipokumbatiwa, ilipata nguvu ambayo ililemaza fikara na kuharibu heshima na utii. Kwa sababu hii, Shetani na wafuasi wake walitupwa kutoka Mbinguni.

**Katika uasi wake, Shetani alionyesha dharau kwa mamlaka ya Mungu, na karibu akanyage kila amri katika sheria yake. Yeye ndiye mfano mkuu wa wakosaji wote**. Kujiingiza katika kutokuamini, kukosa shukrani, uasi, kumuasi Mungu, au uadui dhidi yake, nikurudia tu mkondo ambao shetani alifuata mbinguni. Uasi dhidi ya Mungu ni kama tokeo la moja kwa moja kwa athari ya Shetani kama tendo la uchawi. Kama uchawi, huweka urogi, nguvu ya udanganyifu ambayo hukaribia kutowezekana kuvunjwa. Wale ambao hujiweka dhidi ya utawala wa Mungu wameingia katika muungano na muasi mkuu, na sio rahisi kupoteza windo lake. Nguvu zake zote na ujanja zitafanyishwa kazi kuvutia hisia na kupotosha ufahamu wa waathiriwa wake. Kila kitu huonekana kwao kwa nuru ya uongo. Chini ya uchawi wake huendelea wawezavyo, kama wazazi wetu wa kwanza, huona manufaa makuu ambayo watapokea kwa uasi. Ili kuafikia kitu ambacho wanakusudia, hawatakoma kwa namna yoyote, licha ya hatari kwa wengine au dhambi kwao wenyewe.

**Hakuna ushahidi wenye nguvu zaidi unaweza tolewa kuhusu uwezo wa udanganyifu wa Shetani kuliko ule ambao wengi ambao wanaongozwa naye hujidanganya kwa imani kwamba wako katika huduma ya Mungu. Waandishi na wazee wa Kiyahudi katika siku za Kristo walitangaza jitihada kuu ya kumheshimu Mungu, na bado walimkataa Mwanawe.** Yesu aliwapa ushahidi wenye hitimisho nzuri zaidi kwamba ndiye walioahidiwa. Katika tukio moja, Roho alishuhudia kwa uwezo mkubwa kwa madai yake kiasi ya kwamba mioyo ya wote waliokuwa katika sinagogi waliitikia maneno ya neema zaidi yaliyotoka kwenye midomo yake. Hapo ndipo palikuwa hatua ya kugeuka kwa kundi hilo. Uungu wa Kristo ulipoakisi kupitia ubinadamu, mtazamo wao wa roho uliharakishwa. Uwezo mpya wa utambuzi na kuthamini ukaja juu yao, na hukumu ilikuwa karibu kukosa pingamizi kuwa Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Lakini Shetani alikuwa tayari kuamsha shauku, kutokuamini, na kiburi. Walifanya mioyo yao migumu dhidi ya maneno ya Mkombozi. Walipojitoa kwa mamlaka ya Shetani, walichomwa na hasira isiyoweza kuthibitiwa dhidi ya Yesu. Kwa mkataba mmoja wangeuchukua uzima wake, kama malaika hawangeingilia kwa ukombozi wake.

Roho angali mioyoni mwa wale ambao hujipanga kufuata hukumu zao potovu katika upinzani na mapenzi ya Mungu. Mapambano baina ya kweli na kosa yatadhihirisha kiburi na ukaidi sawa, na chuki sawa isiyo na mantiki dhidi ya watetezi wa kweli, kama ilivyoonyeshwa na Wayahudi wasioamini.

**Yule ambaye anaweza sababisha utukufu wote wa falme za ulimwengu kupita mbele za Kristo katika saa ya kujaribiwa kwake, huonyesha uwezo kama wa uchawi juu ya mawazo ya wote ambao hawamwamini na kumtii Mungu kikamilifu**. Ni kupumbazwa huku kwa maadili ndiko huiba mioyo yao dhidi ya athari ya Roho Mtakatifu. Hili ndilo lilimfanya Korah, Dathani, na Abirami kuasi dhidi ya mamlaka ya Musa. Shetani aliwadanganya na wazo kwamba walikuwa wanapinga kiogozi mwanadamu tu, mtu kama wao tu. Lakini **katika kukataa vyombo teule vya Mungu, walimkataa Kristo, kiongozi wao asiyeonekana**. Walitukana Roho wa Mungu; na hukumu ilifuatia kwa karibu juu ya dhambi yao. Walidanganywa na Shetani, lakini kwa idhini yao wenyewe; kwa sababu walijiweka katika uwezo wake.

Ndivyo ilivyokuwa na Sauli. Alikuwa na ushahidi wazi kabisa ambao Samweli alikuwa amepewa kiungu na kuongozwa na roho. Alikuwa katika upinzani na maagizo yote ya maantiki na uamuzi timamu, kiasi kwamba alianza kukataa maagizo ya Mungu kupitia kwa nabii. **Dhana yake mbaya inaweza husishwa na uchawi huu wa Kishetani, ambao ulimfanya kipofu kwa dhambi, na kutotambua matokeo yake**. Sauli alidhihirisha jitihada kuu ya kuhusuru vinyago na uchawi, akiweka amri kwanza wote ambao watapatikana na hatia ya mambo haya wataadhibiwa kwa kifo. Ingawa nabii anamuonyesha kwamba katika uasi wake wa agizo takatifu **alikuwa akiendeshwa na roho huyo huyo wa upinzani kwa Mungu, na alikuwa kwa uhalisia akiongozwa na Shetani, kana kwamba alikuwa akifanya uchawi**. Na zaidi, alipoonywa, alikuwa ameongeza ukaidi kwa uasi. Badala ya kutubu dhambi yake, na kutafuta msamaha kwa unyenyekevu, alikataa maonyo, na kuufanya moyo wake kuwa mgumu katika uasi. Hangekuwa amefanya chukizo kuu zaidi kwa Roho wa Mungu, kama angekuwa ameunganika na vinyago kwa uwazi.

Ni hatua hatari kutotii mashauri na maonyo ya maneno au Roho wa Mungu. Wengi, kama Sauli, wanasikiza majaribu hadi wanakuwa vipofu kwa tabia halisi ya dhambi. Wanajisifu mno kwamba wanatazamia kitu kizuri, na hawajafanya kosa lolote, kwa kuondoka katika mahitaji ya Bwana. Kwa hivyo wanampuuza Roho wa neema hadi sauti yake ya kusihi haisikiki tena, na wanaachwa kwa udanganyifu ambao wamechagua.

# Kazi ya Sauli

Katika maisha ya Sauli tunaona mazao ya Waisraeil ya kutamani kuwa na Mfalme. Waisraeli walikuwa wamemkataa Mungu kama mtawala wao. Walijitoa kwake na pahali pa uwepo wake walipatiwa dhihirisho la mioyo yao wenyewe.

Wanasema kuwa nguvu huharibu lakini nguvu zaidi huharibu zaidi. Sauli hakupewa nguvu zaidi lakini alitenda kana kwamba alikuwa nazo. Sauli alikataa wito na kukemewa kwa Samweli.

"Lakini kwa kukataa chombo teule cha Mungu, walimkataa Kristo, mtawala asiyeonekana. Walimtukana Roho wa Mungu; na hukumu ilifuata kwa karibu juu ya dhambi zao. Walidanganywa na Shetani, lakini kwa idhini yao wenyewe; kwa sababu walijiweka katika utawala wake."

"Hivyo ndivyo ilivyokuwa na Sauli. Alikuwa na ushahidi wazi zaidi ambao Samweli alikuwa ameteua na kuongoza kwa nguvu za uungu. Alikuwa katika upinzani na amri zote za fikara, na hukumu ya kweli, kwamba alianza kutojali agizo la Mungu kupitia kwa nabii. Dhuluma zake za mauti lazima zihusishwe na uchawi huu wa Kishetani, ambao ulimfanya kipofu kwa dhambi, na kukosa akili kwa athari zake. Sauli alikuwa amedhihirisha jitihada kuu ya kuhusuru ibada ya sanamu na uchawi, akiamuru kuwa wote watakaopatikana wakifanya hivi wataadhibiwa kwa kifo. Ila nabii anamuonyesha kwamba katika kutotii kwake agizo takatifu alikuwa anaendeshwa na roho sawa ya upinzani kwa Mungu, na kwa kweli alikuwa akiongozwa na Shetani, kana kwamba alikuwa akifanya uchawi." ST Sep 14, 1882